Doria ya Neno la Mungu Katika Bara la Afrika



"Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo."
Waebrania 4:12

JERICHO WALLS
PRAYER NETWORK

transformation

Maono

Kutangaza Neno la Mungu katika kila taifa la Kiafrika kwa masaa 24 katika kipindi cha siku 7.

Hamasa

Kuna uelewa mkubwa katika kanisa la Africa kuhusu nguvu ya maombi na maombezi. Pia kuna njaa inayoongezeka kuhusu kukua kiroho, kwa ajili ya ufunuo mpya kuhusu Mungu ni nani; kwa ajili ya uhusiano wa ndani zaidi na Mungu, kwa kuachiliwa upya kwa upako wa Roho Mtakatifu ili kulitakasa, kulitia nguvu na kuliwezesha kanisa katika kizazi chetu na kwa ajili ya mabadiliko dhahiri ya jamii zetu yatokanayo na kishindo cha mwenendo wa kiroho cha wafuasi wa Yesu Kristo waliokomaa kiroho.

Mungu ametoa Neno lake kama nyenzo ambayo Roho Mtakatifu atatumia katika kulileta kanisa katika ushirika kamili na Mungu na makusudi Yake. Neno la Mungu ni mbegu inayotoa tunda la roho (Luka 8:11; 1 Petro.1: 23) na ni upanga wa Roho Mtakatifu unaotumiwa dhidi ya mapepo wabaya katika ulimwengu wa roho na falme na mamlaka (Waefeso 6: 17). Yesu aliwaamuru wafuasi wake kukaa katika neno lake (Yohana 8:31). Tunda la kukaa katika Neno la Mungu ni kusafishwa (Zaburi 119: 9; Yohana 15:3; Waefeso.5: 26), uamsho (Zaburi.119:25), kukua kwa imani (Warumi 10:17); utakaso (Yohana 17:17; Waefeso 5:26), kufunguliwa (Yohana 8:3; 17:17) na uhusiano wa ndani sana na Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu (Yohana 14:23).

Kusudi

Makusudi mawili ya Doria hii ya Neno la Mungu hili la Neno ni: Kutangaza kwa sauti Neno la Mungu juu ya Bara la Afrika na kuchochea kwa upya uelewa wa nguvu ya kuomba kwa kutumia Neno la Mungu.

Kielelezo halisi cha nguvu ya kusoma Neno la Mungu kinapatikana katika Nehemia 8:13 – 9:38. Baada ya uhamishoe wa Babeli, mabaki ya Wayahudi waliorejea Yerusalemu kwanza walijenga *madhabahu ya matoleo*, wakakarabati hekalu na wakaanzisha ibada ya kuabudu kila siku. Kisha wakajenga ukuta kuunzunguka Yerusalemu. Wakati wa kuuweka wakfu ukuta waliadhimisha sikukuu ya vibanda na wiki nzima Ezra, kuhani, aliwasomea watu neno la Mungu. Jambo hili lilifuatiwa na kipindi muhumi sana katika historia ya Israeli cha toba na kutakaswa.

Mwongozo wa Msingi wa Jinsi ya Kushika Zamu kwa Masaa 24 kwa Siku 7

- Kila mtu atakayeshiriki atawajibika kwa saa moja kila siku kusoma Neno kama tamko la kinabii,. Itakuwa vizuri zaidi akisoma kwa sauti.
- Itakuwa vyema kuwa na kituo kimoja cha kukutania, ambapo washiriki watakuja kusoma neno.
- Kwa masaa 6 kwa siku Zaburi itasomwa (masaa 3 asubuhi na masaa 3 jioni kama ishara ya asubuhi na jioni ya dhabihu za sifa. Hii ina maana kwamba kila siku kitabu kizima cha Zaburi kitatumiwa kuombea). Katika muda uliosalia (masaa 18) neno litasomwa, kuanzia kitabu cha Mwanzo na kuishia Ufunuo.
- Kila saa itaanzia na:
    - Maombi binafsi (angalia ukurasa wa 4) kwamba neno limbariki mtu binafsi, na
    - Tamko la Neno kimaombi (angalia ukurasa 5-52) kabla ya mshiriki hajaanza sehemu yake ya kusoma Neno.
- Uwe na kitabu cha kurekodi wapi kila mtu ataanza kusoma na wapi atamalizia katika mwisho wa saa lake la doria/kukesha ili anayefuata aendelee mahali pale alipomalizia.
- Ikiwa wawili au zaidi wameamua kushirikiana katika saa mmoja, wanaweza kupokezana kusoma sura hizo au watumie tafsiri moja ya biblia kusoma kwa sauti pamoja. Kwa wale wasio weza kusoma hakuna haja ya kuwatenga, kwa kuwa kusikia neno ni baraka pia.
- Kama una washiriki wengi, fikiria kuwa na vyumba vya ziada au tayarisha sehemu nyingine ya kusomea Neno katika kijiji au jiji. Kama unawashiriki wachache, fikiria kutumia kanda ya biblia kwenye kaseti au cd kufidia masaa ambayo hayajachukuliwa.
- Ubunifu wa ziada wa mahali pa maombi, unaweza kutayarisha meza na kiti ndani ya soko, au dukani au sehemu nyingine ya makutanio na usome Neno kwa sauti ili kwamba wapita njia wasikie Neno la Mungu. Kama una washiriki wanaoweza kutembea unaweza pia kuweka hema katika kilima au mlima unaotazama mji na usome Neno ukielekea mji.
- Kijitabu hiki na mwongozo wa maombi ni ushauri tu. Uwe huru kutumia njia zingine bunifu za kutangaza Neno la Mungu katika jamii yako.

Mwongozo huu unapatikana katika internet kwa Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa, Kireno na Kiswahili. Tafsiri katika lugha nyingine zinakaribishwa. Tafadhali wasiliana na Jericho Walls International Prayer Network kwa habari zaidi: info@jwipn.com au tembelea tofuti yetu: www.jwipn.com ambapo unaweza kunakili Mwongozo huu.

Maombi binafsi

Tumia dakika moja au mbili kutuliza moyo na ufahamu wako mbele za Kiti cha Neema.

- “Mungu Baba, katikaJjina la Yesu Kristo, nakuja kwa ujasiri kwenye kiti chako cha Neema.”

- “Bwana Yesu Kristo, naiweka mizigo yangu yote mbele Zako.”

- “Roho Mtakatifu, tafadhari uniongoze na unibariki ninaposoma Neno.”

- “Mungu Baba, Nafungua moyo na ufahamu wangu kupokea ufunuo toka kwako. Tafadhari unifunulie pia chochote kitakachonizuia kusikia sauti Yako.”

- “Bwana Mungu, najito Kwako niwe dhabihu iliyo hai na kama chombo cha kutumiwa na Roho Mtakatifu.”

Subiri mpaka utakapoingia katika uwepo wa Mungu kabla ya kuendelea na kipindi cha maombi. Maliza kusoma neno dakika 5 kabla ya mwisho wa kipindi chako cha saa moja. Tumia dakika hizi za mwisho kufurahia uwepo wa Mungu na uandike yale uyaonayo, maneno au maono katika kitabu cha kurekodia.

Saa ya Kwanza: Saa 6 – 7.00 Usiku

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendeleana usomaji wa Biblia)

Usomaji wa Biblia: Soma kutoka Mwanzo hadi Ufunuo – Angalia daftari lako la kumbukumbu kuhusu mahali pa kuanzia kusoma Neno

Lengo la tamko hili ni: Nguvu ya Jina la Mungu

Baba yetu wa Mbinguni, Uliyetukuka, Ukaaye milele, ambaye jina lake ni Mtakatifu (Isaya.57:15). Jina lako litukuzwe na liabudiwe (Mathayo.6:9). Tunakushukuru kwa kumbukumbu la utakatifu wa Jina lako (Zaburi.30:4). Tunakuimbia na kulisifu jina lako, na kuwajulisha watu matendo yako (Zaburi.68: 4; 105:1). Umetujulisha Jina lako la ahadi, Kwa Ibrahimu kwanza na kwa Israeli: Yahweh El Shaddai, Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo (Ex.3:13-15; 6:3). Maana Wewe ndiwe Baba Yetu; mkombozi wetu tangu milele (Isaya.63:16). Umetufunulia Ubaba wako, kupitia mwanao, Yesu Kristo (Yohana 14:9; 17:6,26). Kwasababu Yesu alitii na kujinyenyekesha hata mauti, naam mauti ya msalaba, Umemwadhimisha mno, ukamkirimia Jina lile lipitalo kila jina. Ili kwa Jina la Yesu kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA (Wafilipi.2:9). Umetupatia Jina lake kuliitia kwa wokovu wetu na hivyo tunakulilia, utuokoe, Ee Mungu, kwa Jina la Yesu! (Matendo 4:12; Matayo.1:21; Zaburi.54:1; Yoeli.2:32)

Umetuamuru tusilitaje bure Jina lako, wala kulinajisi au kulikufuru Jina lako (Kutoka.20:7; Walawi.19:12; 24:16). Jina lako limetiwa unajisi katika mataifa na watu wengi wamelisahau Jina lako na wamemnyoshea Mungu mgeni mikono yao (Ezekieli.36:23. Zaburi. 44:20). Tunakiri tumevunja amri yako. Tunapoomba na kukiri Jina loka, na kuacha dhambi yetu, usikie na kuturejesha (2 Nyakati.6: 32,33). Utusamehe, na ulitakase Jina lako kuu ili mataifa,, hata maadui zako, wajue yakuwa wewe ndiwe Bwana na wa kuche wewe (Ezekieli.36:21,23; Isaya.64:2; Zaburi.102:15).

Ee Bwana, Mungu wetu, mabwana wengine zaidi ya wewe wametumiliki; lakini kwa msaada wako peke yako tutalitaja jina lako (Isaya.26:13). Tumebatizwa kwa Jina lako na umetupa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu (Mathayo.28: 19; Yohana 1:12). Na kwa kuamini tunauzima kwa jina Lako (Yohana 20:31). Shauku ya nafsi yangu inaelekea Jina lako na ukumbusho wako (Isa.26:8) Wakati wa usiku nimelikumbuka Jina lako na kulitafakari (Zaburi.119:55; Malaki.3:16). Moyo wangu na ufurahi kulicha Jina lako ili niuache uovu na kulishika sana Jina lako na kutolikana Jina lako (Zaburi.86:11; 2 Timotheo.2:19; Ufunuo. 2:13; 3:8). Jina lako ni la ajabu, ni kama marhamu iliyomiminwa, ni ngome imara mwenye haki huikimbilia, akawa salama (Waamuzi 13:18; W.Ulio bora.1: 3; Mithali.18:10; Zaburi.61:3).

Kwa Jina Lako tutapigana vita dhidi ya maadui zako kwani Jina Lako litatulinda (1 Samweli.17:45; Zaburi.20:1). Hatuta weka tumaini letu katika nguvu za kijeshi, lakini tutalikumbuka/litaja Jina Lako kwasababu msaada wetu upo katika Jina la Bwana wetu, aliyezifanya mbingu na nchi (Zaburi.20: 7; Zaburi.124:8). Nao wakujuao Jina Lako, wakutumaini wewe na kulingojea Jina lako (Zaburi.9: 10; Zaburi. 52:9). Mnyonge na mhitaji na walisifu Jina Lako (Zaburi.74:21). Kwetu sisi tunaolicha Jina Lako jua la haki lituzukie, lenye kuponya katika mbaya zake. (Malaki.4: 2).

Ndivyo nitakavyokubariki maadamu ni hai; Kwa Jina lako nitaiinua mikono yangu na kulitukuza Jina lako (Zaburi.63:4; 115:1), na kinywa changu kitazinena sifa za Bwana, wote wenye mwili na walihimidi Jina lako takatifu milele na milele! (Zaburi.145:21). Jina lako tukufu na lihimidiwe milele, dunia yote na ijae utukufu wako! (Zaburi.72:19). Toka maawio ya jua, hata machweo yake Jina la Bwana husifiwa, na Jina lako Mataifa watalitumainia! (Malaki.1:14; Mathayo.12:21). Ee Bwana, Jina lako ni la milele, kumbukumbu lako vizazi hata vizazi! (Zaburi.135:13). Amebarikiwa ajaye kwa Jina la Bwana! (Mathayo.23:39)

Saa ya 2: Saa 7:00 - 8:00 Usiku

(Omba maombi yako binafsi na utoe mwelekeo wa tangazao hili kabla ya kuendeleana usomaji wa biblia)

Usomaji wa Biblia: Soma toka Mwanzo hadi Ufunuo – angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Neema na Rehema za Mungu

Ee Baba wa rehema uyaelekee maombi yetu na ombi letu la rehema (1Wafalme 8:28). Kama vile macho ya watumishi kwa mkono wa bwana zao; Kama macho ya mjakazi ka mkono wa bibi yake; Hivyo macho yetu humlekea Bwana, Mungu wetu, Hata atakapoturehemu (Zaburi.123:2). Tunakikaribia kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji (Waebrania.4:16; Zaburi.5:7; 6:9; 28:2). Nawe, Bwana, usinizuilie rehema zako, fadhili zako na kweli yako na zinihifadhi daima (Zaburi.40:11). Maana mbingu zilivyoinuka juu ya nchi, kadiri ile ile rehema zake ni kuu kwa wamchao. Wewe ni mwema na rehema zako hudumu vizazi hata vizazi kwa hao wanaomcha (Zaburi.103:11,17; 106:1; Luka 1:50). Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi; wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe; mwenye kuwapatiliza wwatoto uovu wa baba zao, na wana wa wana wao pia, hata kizazi cha tatu na cha nne. Wewe Bwana ni mwema kwa watu wote, na rehema zako zi juu ya kazi zako zote (Kutoka.34:6-7; Zaburi.145:9). Ni kwa sababu ya ya huruma zako Bwana kwamba hatuangamii; kwakuwa rehema zako hazikomi. Maana ujapomhuzunisha utamrehemu, kwa kadiri ya wingi wa huruma zako (Maombolezo.3:22,32). Katika ukuu wako ulitamka: “Nami nitamfadhili yeye nitakayemfadhili; nitamrehemu yeye nitakayemrehemu.” (Kutoka.33:19; Warumi.9:16,18). Nawe, Bwana, usituzuilie rehema zako, fadhili zakona kweli yako na zituhifadhi daima (Zaburi.40:11). Mungu wa rehema, utuponye roho zetu maana tumekutenda dhambi kiasi cha wingi wa rehema zako uyafute makosa yetu (Zaburi.41:4; 51:1). Tunapoficha dhambi zetu hatutafanikiwa, hivyo tunaunama na kuziacha ili tupate rehema zako (Mithali.28:13). Usikumbuke juu yetu maovu ya baba zetu; rehema zako zije kutulaki hima, kwa maana tumedhilika sana (Zaburi.79:8).

Ni nani aliye Mungu kama wewe, mwenye kusamehe uovu, na kuliachilia kosa la watu wa urithi wake waliosalia? Hashiki hasira yake milele, kwa maana yeye hufurahia rehema? (Mika.7:18). Uwarehemu watu wa mataifa, kama ulivyo rehemu Israeli. Usiwakomeshe kabisa, wala kuwaacha, kwa maana wewe u Mungu mwenye neema, mwenye rehema. Uwape wale wasiopata rehema yako

sasa, ili wakutukuze (Nehemia.9:31; 1 Petro.2:10; Warumi.15:9). Bwana Yesu Kristo, Ulikuja ulimwenguni kuwaokoa wenye dhambi, sasa onyesha rehema zako kwa waliopotea na mataifa yaliyofungwa na nguvu za mapepo na kutokujua wokovu mkuu uliofunuliwa kwao, katika ghadhabu kumbuka rehema (1 Timotheo.1: 16; Habakuki.3:2).

Baba, Unapendezwa na fadhili, wala si sadaka, na kumjua Mungu kuliko sadaka za kuteketezwa (Hosea.6:6). Umetuonyesha yaliyo mema; na wewe Bwana unataka nini kwetu, ila kutenda haki na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wetu (Mika.6:8). Tutie nguvu kufanya mapenzi yako; utusaidie kufuata mfano wako kufanya hukumu ya kweli, kila mtu na amwonee ndugu yake rehema na huruma “Heri wenye rehema; maana hao watapata rehema.” (Zekaria.7:9; Mathayo.5:7; Warumi.12:18). Huruma na ijitukuze juu ya hukumu katika maisha yetu (Yakobo 2:13). Tunaomba kanisa ambalo litapanda haki, na kuvuna kwa fadhili (Hosea.10: 12). Tusiache mambo makuu ya sheria, yaani adili, na rehema (Mathayo.23:23). Haki na hukumu ndio msingi wa kiti chako, fadhili na kweli zahudhuria mbele za uso wako. (Zaburi.89:14; 85:10).

Kwa sababu ya huruma zako, tunatoa miili yetu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kukupendeza. Pokea ibada yetu yenye maana (Warumi.12:1). Pamoja na kanisa vizazi vyote tunapaza sauti zetu: Bwana wetu Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai, uturehemu (Mathayo.9:27; Luka 18:38; Mathayo 15:22). Tuongezee rehema na amani na upendo (Yuda2). Hakika wema na fadhili zitatufuata siku zote za maisha yetu nasi tukaa nyumbani mwa Bwana milele (Ps.23:6).

Saa ya 3: Saa 8:00 – 9:00 Usiku

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea na usomaji wa biblia)

Usomaji wa Biblia: Soma kutoka Mwanzo hadi Ufunuo – angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Kuabudu kutoka katika maombi ya mitume

Jinsi zilivyo kuu utajiri na hekima na maarifa ya Mungu! Hukumu zake hazichunguziki, wala njia zake hazitafutikani! Maana ni nani aliyeijua nia na Bwana? Au ni nani aliyekuwa mshauri wake? Au ni nani aliyempa yeye kitu kwanza, naye atalipwa tena? Kwa kuwa vitu vyote vyatoka kwake, viko kwa uweza wake, tena vinarejea kwake. Utukufu una yeye milele. Amina (Warumi.11:33-36). Sasa kwa Mfalme wa milele, asiyeweza kuona uharibifu, asiyeonekana, Mungu peke yake, na iwe heshima na utukufu milele na milele. Amina (1 Timotheo.1:17). Tunakubariki Mungu wetu, mtawala pekee, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana, ambaye yeye peke yake hapatikani na mauti, amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa; wala hakuna mwanadamu aliyemwona, wala awezaye kumwona. Heshima na uweza una yeye hata milele. Amina. (1 Timotheo.6:15-16).

Bwana, tunatangaza kwamba hapo mwanzo, uliitia ya nchi, na mbingu ni kazi za mikono yako; Hizo zitaharibika, bali wewe unadumu; nazo zote zitachakaa kama nguo, na kama mavazi utazizinga, nazo zitabadilika; Lakini wewe u yeye yule, na miaka yako haita koma. (Waebrania.1:10-12). Mola, wewe ndiwe Mungu, ndiwe uliyefanya mbingu na nchi na bahari na vitu vyote vilivyomo; nawe ulinena kwa Roho Mtakatifu kwa kinywa cha baba yetu Daudi, mtumishi wako, mbona mataifa wamefanya ghasia, na makabila wametafakari ubatili? Wafalme wa dunia wamejipanga, na wakuu wamefanya shauri pamoja juu ya Bwana na juu ya Kristo wake.Kama ilivyokuwa siku za Herode na Pontio Pilato, hata leo watu wanao pinga injili, wanakusanyika juu ya mtumishi wako mtakatifu Yesu, ulilyemtia mafuta. Basi sasa, Bwana yaangalie matisho yao; upinzani na kuzuiliwa na serikali na watu wasioelewa na waovu na mashirika, lijalie kanisa, kila mkristo kunena neno lako kwa ujasiri wote, ukinyosha mkono wako kuponya; ishara na maajabu vifanyike kwa jina la Mtumishi wako mtakatifu Yesu.” (Matendo 4:23-31).

Utukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo; kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo. Kwa kuwa alitangulia

kutuchagua, ilitufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake – na usifiwe utukufu wa neena yake, ambayo ametuneemesha katika huyo Mpendwa. Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi sawasawa na wingi wa neema yake naye alituzidishia hiyo katika hekima yote na ujuzi; akiisha kutujulisha siri ya mapenzi yake, sawasawa na uradhi wake, alioukusudia katika yeye huyo. Yaani kuleta madaraka ya wakati mkamilifu atavijumlisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vity vya duniani pia. Naam, katika yeye huyo mwanao Yesu Kristo. Na ndani yake sisi nasi tulifanywa urithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye, ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake. Nasi katika huyo tupate kuwa sifa ya utukufu wake, sis tuliotangulia kumwekea Kristo tumaini letu. Ahsante Baba kwakuwa nasi pia katika huyo tumekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wetu tena tumekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu. Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi wa milki yake kuwa sifa na utukufu wake. (Waefeso.1:3-14).

Saa ya 4: Saa 9:00 -10:00 Usiku

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea na usomaji wa biblia)

Usomaji wa Biblia: Soma kutoka Mwanzo hadi Ufunuo – angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Maombi ya kukua kiroho

Baba wa Bwana Yesu Kristo, tafadhari tufunulie siri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake. Unapenda kutujulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu. Tufariji mioyo yetu na utuunganishe katika upendo, na waumini wengine, tukapate utajiri wote wa kufahamu kwa hakika, wapatekujua kabisa siri ya Mungu yaani, kristo; ambaye ndani yake yeye hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika. **Amina.** (Wakolosai 1:26-27; 2:2-3)

Kristo Yesu, Bwana wangu, nayahesabu mambo yote kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa jumjua Kristo Yesu, Bwana wangu; ambaye kw ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nipate Kristo; tena nionekane katika yeye nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatiknayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani. Ili nikujue wewe, na uweza wa kufufuka kwako, na ushirika wa mateso yako, nikafananishwe na kufa kwako. Ili nipate kwa njia yo yote kuifikia kiyama ya watu, Si kwamba nimekwisha kufika, au nimekwisha kuwa mkamilifu; la bali nakaza mwendo ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu. Sijdhanii nasfi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu. **Amina.** (Wafilipi 3:8-14)

Baba wa Bwana Yesu Kristo, Ninaomba utujaze maarifa ya mapenzi yako katika hekima yote na ufahamu wa rohoni; tuenende kama ilivyo wajibu wetu kwa Bwana, tukimpendeza kabisa, tukizaa matunda kwa kila kazi njema, na kuzidi katika maarifa ya Mungu; tukiwezeshwa kwa uwezo wote, kwa kadiri ya nguvu ya utukufu wako, tupate kuwa na saburi ya kila namna na uvumilivu pamoja na furaha. Nakushurkuru baba uliye tustahilisha kupokea sehemu ya urithi wa watakatifu katika nuru. Nawe ulituokoakatika nbguvu za giza, ukatuhamisha na kutingiza katika ufalme wa msamaha wa dhambi. **Amina.** (Wakolosai 1:9-14)

Baba kwa ujasiri tunaomba kwamba wewe uliyeanza kazi njema mioyoni mwetu utaimaliza hata siku ya Kristo Yesu. Kama tunavyo shiriki katika neema yako.

Pendo letu lizidi kuwa jingi sana, katika hekima na ufahamu wote, tupate kuyakubali yaliyo mema; ili tupate kuwa na mioyo safi, bila kosa, mpaka siku ya Kristo, hali tumejazwa matunda ya haki, kwa njia ya Yesu Kristo, kwa utukufu na sifa ya Mungu (Wafilipi.1:6-11). Katika Jina la Yesu Kristo tunakataa kujisumbua kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba pamoja na kushukuru, haja zetu na zijulikane nawe Bwana wetu na Mungu, pia tunaomba amani ya Mungu, ipitayo akili zote ituhifadhi mioyo yetu na nia zetu kaitka Kristo Yesut (Wafilipi.4:6-7). Mungu wewe ni mpaji wetu na tunaomba utujaze kila tunachohitaji kwa kadiri ya utajiri wako, katika utukutu ndani ya Kristo Yesu. Sasa atukuzwe Mungu, Baba yetu, milele na milele. **Amina** (Wafilipi.4:19-20).

Mungu wa amani mwenyewe atutakase kabisa; nasi nafsi zetu na roho zetu na miili yetu ihifadhiwe tuwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesut Kristo. Wewe ni mwaminifu ambaye umetuita, nawe utafanya. Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo na iwe pamoja nasi (1 Wathesalonike.5:23-25, 28). Wewe uwezaye kutulinda sisi tusijikwae, na kutusimamisha mbele ya utukufu wako bila mawaa katika furaha kuu. Wewe uliye Mungu pekee, Mwokozi wetu kwa Yesu Kristo Bwana wetu; utukufu una wewe, na ukuu, na uwezo, na nguvu tangu milele, na sasa, na hata milele. **Amina**. (Yuda 1:24,25).

Saa ya 5: 04:00 – 05:00 Alfajiri

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea usomaji wa biblia)

Usomaji wa Biblia: Soma kutoka Mwanzo hadi Ufunuo – angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Masuala la Ardhi (1): Umiliki wa Ardhi

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi, aliyekuwako na aliyeko na atakayekuja! (Ufunuo.4:8). Umestahili wewe, bwana wetu na Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza; kwa kuwa wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako, navyo vikaumbwa (Ufunuo.4:11). Hapo mwanzo Mungu uliziumba mbingu na nchi. Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji na Ukasema “Iwe nuru!” ikawa nuru (Mwanzo.1:1-3). Ndiyo, hapo mwanzo kulikuwapo Neno naye Neno alikuwako kwa Mungu naye Neno alikuwa Mungu, Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu, vyote vilifanyika kwa huyo; pasipo Yeye hakukufanyika chochote kilichofanyika, ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu. Nayo nuru yang’aa gizani nalo giza halikuiweza (Yohana.1:1-5). Wewe ndiwe BWANA, wewe peke yako; wewe ulifanya mbingu, mbingu za mbingu, pamoja na jeshi lako lote, dunia na vyote vilivyomo, bahari na vitu vyote vilivyomo, nawe unavihifadhi vitu hivi vyote; na jeshi la mbinguni lakusujudu wewe (Nehemia.9:6).

Wewe, Bwana Mungu, uliiweka mipaka yote na dunia, kaskazini na kusi Wewe ulizitengeneza (Zaburi 74:17), na uliahidi kwamba muda nchi idumupo, majira ya kupanda, na mavuno wakati wa baridi na wakati wa hari, wakati wa kaskazi na wakati wa kusi, machana na usiku, havitakoma. (Mwanzo.8:22). Hukuiumba dunia ukiwa, uliiumba ili ikaliwe na watu! (Isaya.45:18) Umeijaza dunia, na bahari na hewa kwa mimea na viumbe hai (Mwanzo.1:11-12; 20-25). Umemuumba mwanadamu, mwanamme na mwanamke, kuwa wawakilishi wako duniani, wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi (Mwanzo.1:26). Wewe umewapa pumzi watu walio juu yake; wewe uwapaye roho wao waendao ndani yake (Isaya.42:5; Mwanzo.2:7).

Uliwapa wanadamu chakula chao – kila mche utoao mbegu, na kila mti ambao matunda yake yana mbegu; na kila kitambaacho juu ya nchi, chenye uhai, Umetupatia kama chakula tule (Mwanzo.1:29; 9:3; Kum ya Torati.12:15). Ni wewe, Bwana Mungu utupaye umande wa mbingu, na ya manono ya nchi, utoae

wingi wa nafaka na mvinyo. Unaifurahisha mioyo yetu na divai, Unatupatia mafuta tuung'aze nyuso zetu, na mkate kuburudisha mioyo yetu (Mwanzo.1:11; 27:28; Zaburi.104:14,15). Ni wewe, Bwana Mungu, unayemwagilia nchi na kuitayarishia mvua. Unatupa mvua kwa wakati wake, mvua ya masika na mvua ya vuli (Zaburi.65:9; 147:8; Kum la Torati.11:14.) Umejaza nchi na mema yako. Umetupa pia mawe yenye dhamani kutoka katika nchi, ili tukutukuze wewe kwa nchi nzuri uliyotupa (Kum la Torari.8:7-10). Nchi imejaa fadhili za BWANA (Zaburi 33:5) dunia yote imejaa utukufu wake (Isaya.6:3).

Bwana Mungu, dunia yote ni mali yako kwasababu ulikuwepo kabla hujaiumba dunia (Zaburi.90:2) Ni wewe pekee uliye husika kuwepo kwa dunia hii (Kutoka.9:29; Zaburi 24:1). Umetamalaki/ unatawala dunia yote (Zaburi.97:1), nchi umewapa wanadamu kama maeneo ya kuishi na kutawala (Zaburi.115:16; Mwanzo.1:26). Lanini unajua kila kitu kinacho tokea katika dunia hii (Zekaria.4:10; Zaburi.33:13), ukimchunguza mbaya na mwema (Mithali.15:3). Wala hakuna kiumbe kisichokuwa wazi mbele zako, lakini vitu vyote vi utupu na kufunuliwa machoni pako na tutawajibika kwako (Waebrania.4:13). Tunapo simama mbele zako sasa tunakiri kwamba mwanadamu ameshindwa katika jukumu lile ulilotupa. Dunia imewtiwa ufisadi na kunajisika kwasababu ya dhambi zetu ha uasi wetu kwako (Mwanzo.6:11-12; Isaya.24:4-6). Uturehemu tafadhali kwakuwa sisi watoto wako tunakugeukia tuki sihi utukomboe (Warumi.8:19-23).

Saa ya 6: 05:00 – 06:00 Alfajiri

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea na usomaji wa biblia)

Usomaji wa Biblia: Soma kutoka Mwanzo hadi Ufunuo – angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Masuala ya Ardhi (2): Toba kwa ajili ya umwagaji damu na ibada za sanamu

Bwana Mungu, uliye mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi (Ex.34:6,7). Nawe ulifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, wakae juu ya uso wa nchi yote, akiisha kuwawekea nyakati alizosiamuru tangu zamani, na mipaka ya makazi yao; ili wakutafute (Kum la Torati.32:8; Matendo17:26,27).

Uturehemu kwakuwa mahali penye giza katika nchi pamejaa makao ya ukatili na dunia yote imeharibika na imenajisika na dhambi (Zaburi.74:20; Mwanzo.6:11,12; Isaya.24:12). Ardhi inatoa michongoma na miiba na inatapika wenyeji wake na kuwatoa (Mwanzo.3:17,18; Walawe.18:25-28). Ardhi zetu zimejaa uhalifu wa kumwaga damu, miji yetu midogo na mikubwa imejaa maasi na maovu na sisi na vizazi vilivyopita hatukudhamini uhai uliotupa (Ezekieli.7:23; Habakuki.2:12). Kwasabubu ya umwagaji damu, mauaji, vita na utoaji mimba, watu wengi wamekuwa wakitangatanga na kuwa wakimbizi (Mwanzo.4:11,12). Ardhi imelaaniwa na tunapolima haitupi mazao yake; na mbingu zetu zilizo juu ya kichwa chetu zimekuwa shaba, na nchi iliyo chini yetu imekuwa chuma (Mwanzo.4:12; Kum la Torati.28:23; Zaburi.107:34). Unachukizwa na mikono imwagayo damu isiyo na hatia, na tuombapo maombi mengi hutasikia; mikono yetu imejaa damu (Mithali.6:17; Isaya.1:15; 59:2). Ulisema uhai wa mtu uko katika damu na damu ya ndugu yako inakulilia kutoka katika ardhi (Mwanzo.4:10; Walawi.17:11). Lakini tunakushukuru kwa damu iliyonyunyizwa ya Yesu Kristo katika madhabahu ya mbinguni inenayo mema kuliko ile ya Habili (Waebrania.12:24). Bwana, Mkombozi wetu tusamehe tafadhali kwa damu zote zilizomwagwa katika mataifa yetu, ondoa laana itokanayo na umwagaji damu kutoka katika ardhi zetu, uitakase damu yetu ambayo hujaitakasa;kwa maana BWANA wewe ndiye ukaaye sayuni, utuoshe kabisa na uovu wetu, ututakase dhambi zetu (Yoeli 3:21; Zaburi.51:2,14). Wewe huvikomesha vita, unafanya hukumu na unakemea mataifa (Zaburi.46:9; Mika.4:3). Uturehemu na uuthibitishe ufalme wako hapa duniani ili mfalme wa amani apate kutawala. Na mamlaka yako yatakuwa toka bahari hata bahari, na toka Mto hata miisho ya dunia (Isaya.9:6,7; Zekaria.9:10; Warumi.14:17).

Bwana wa majeshi, Mungu wa Israeli ukaaye juu ya makerubi, wewe, naam wewe peke yako, ndiwe Mungu wa falme zote za dunia. Wewe ndiwe uliyeziumba mbingu na nchi. (Isaya.37:16). Wala hapana Mungu zaidi yako, Mungu mwenye haki, mwokozi (Isaya.45:21). Kabla hujaumba dunia na tangu milele hata milele ndiwe Mungu (Zaburi.90:2). Kwa sababu mambo yako yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zako (Warumi.1:19,20). Lanini walipomjua Mungu hawakumtukuza kama ndiye Mungu wala kumshukuru Mungu; bali walipotea katika uzushi wao, na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza. Sisi na vizazi vilivyopita tulibadili kweli ya Mungu kuwa uongo, tukavisujudia viumbe na kuviabudu badala ya Muumba anayehimidiwa milele (Warumi.1:21,25). Sisi wote tulimnyoshea mungu mgeni mikono yetu (Zaburi.44:20). Kupitia ibada zetu za sanamu, tamaa na na kujiabudu wenyewe, tumeinajisi ardhi (Wakolosai.3:5; Zaburi.106:38; Ezekieli.22:4; 36:18). Ulisema msifanye sanamu yo yote, wala msijisimamishie sanamu ya kuchonga, wala mnara, wala msiweke jiwe lo lote lililochorwa katika nchi yenu ili kulisujudia; kwa kuwa wewe ndiwe BWANA Mungu wetu (Walawi.26:1). Sasa Ee Bwana, tunavuna matunda ya dhambi zetu. Ukame umetuadhiri, njaa imeshambulia watu wetu, vita vinabiganwa kati ya mataifa yetu madhara ya mazingira yameharibu ardhi yetu kwa sababu tumefarakana nawe na kwenda mbali nawe kama vile tuliona dhuluma kwako! (Ezekieli.14:12-21; Yeremia.2:5) Ee Bwana wangu nimetahayari, naona haya kuinua uso wangu mbele zako, Mungu wangu; kwa maan maovu yetu ni mengi, hata yamefika juu ya vichwa vyetu, na hatia yetu imeongezeka nakufika mbinguni. (Ezra 9:6,7). Tumetenda dhambi pamoja na baba zetu, tumetenda maovu, tumefanya ubaya, turehemu na utusamehe sisi dhambi zetu (Zaburi.106:6). Ututakase na uchafu wetu wote, na vinyago vyetu vyote (Ezekieli.36:25,26). Yaondoe majina ya miungu mingine vinywani mwetu, liinue kanisa safi lisilo na doa ambalo litaonyesha hekima yako iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho (Hosea.2:17; Waefeso.3:10). Heri taifa ambalo BWANA ni Mungu wao! (Zaburi.33:12)

Saa ya 7: Saa 12:00 – 1:00 Asubuhi

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea na usomaji wa biblia)

Usomaji Biblia: Saa la kwanza la kusoma Zaburi - angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Masuala ya Ardhi (3): Toba ya dhuruma, kuvunjika kwa maagano na uasherati/uzinzi

Mungu mwenyezi na Baba wa Bwana na wetu Yesu Kristo, tunalitangaza Jina la Bwana; na kukupa ukuu Mungu wetu. Wewe Mwamba, kazi yako ni kamilifu; njia zako zote ni haki. Mungu wa uaminifu, usiye na uovu, Wewe ndiwe mwenye haki na adili (Kum la Torati.32:3,4). Haki na hukumu ndio msingi wa kiti chako fadhili na kweli zahudhuria mbele za uso wako (Zaburi.89:14,15). Huwafanyia yatima na mjane hukumu ya haki, nawe humpenda mgeni, akimpa chakula na mavazi (Kum la Torati.10:18). Nchi imejaa fadhili za BWANA. (Zaburi 33:5). Umetuonyesha yaliyo mema; na BWANA anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako (Mika.6:8). Na tuliposhindwa kuitunza sheria, ulimtuma mwanao mwenyewe katika mfano wa mwili, ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili, ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya roho (Warumi 8:3,4).

Hakimu wa dunia yote, tunakuja kwako kusihi rehema na neema kwa kizazi chetu hiki. Hukumu ya haki I mbali nasi, twatazamia nuru, na kumbe! Latokea giza! Twapapasa-papasa kutafuta ukuta kama kipofu. Maana makosa yetu yamezidi kuwa mwengi mbele zako, na dhambi zetu zashuhudia juu yetu;maana makosa yetu tunayo pamoja nasi, na maovu yetu tumeyajua, katika kukosa na kumkana BWANA, na katika kugeuka tusimfuate Mungu wetu, tukinena jeuri na uasi, na kukusudia maneno ya uongo na kuyatoa moyoni. Na hukumu imegeuka ikaenda nyuma, na haki inasimama mbali sana; maana kweli imeanguka katika njia kuu, na unyofu hauwezi kuingia, Naam, Iweli imepunguka kabisa, na yeye auachaye uovu ajifanya kuwa mateka; naye BWANA akaona hayo, akachukizwa kwa kuwa hapana hukumu ya haki. (Isaya.59:9-15). Dunia ipo katika huzuni na imenajisika kwa hao waishio ndani yake, Kwasababu wameasi sheria zako na kuvunja agano nawe. Hivyo laana imeiangukia dunia (Isaya.4:3-6). Hapana kweli, wala fadhili wala kumjua Mungu katika nchi. Hapana neno ila kuapa kwa uongo, na kuvunja ahadi, na kuua, na kuiba, na kuzini; huruka mpaka, na damu hugusana na damu (Hosea.4:1-2). Tunajenja nyumba zetu kwa uovu na udhalimu tunatumia watumishi wa wengine bila ujira (Yeremia 22:13). Miji yetu mingi imethibitishwa kwa uovu (Habakuki.2:12). Sheria zetu ni dhalimu na amri

zetu ni za ukandamizaji, ili kumpotosha mhitaji asipate haki yake, na kuwanyang'anya maskini wa watu wangu haki yao; ili wajane wawe mateka yao, na kuwafanya yatima waliofiwa na baba zao kuwa mawindo yao (Isaya.10:2).

Tumetia unajisi ardhi kwa talaka, kwa vitendo vichafu vya ngono kama usenge, zinaa ya maharimu, uasherati na umalaya (Yeremia.3:1-3; Warumi.1:26,27; Walawi.18:23). Tunakiri kwamba kizazi chetu kimejawa na udhalimu wa kila namna, uovu na tamaa na ubaya; tumejawa na husuda, na uuaji, na hadaa; watu wa nia mbaya, wenye kusengenya; Ni wenye kusingizia, wenye kumchukia Mungu, wenye jeuri, wenye kutakabari, wenye majivuno, wenye kutunga mabaya, wasio watii wazazi wao, wasio na ufahamu, wenye kuvunja maagano, wasiopenda jamaa zao, wasio na rehema (Warumi 1:29-31). Hata katika kanisa lako tunakiri kwamba tumenajisi miili yetu kwa uasherati na uzinzi hivyo tumelinajisi hekalu la Roho Mtakatifu (1Wakorintho.6.18-20). Tunakubari kwamba tunahatia mbele zako.

Umeona udhalimu, ukastaajabu kwa kuwa hapana mwombezi; basi mkono wake mwenyewe ndio uliomletea wokovu; na haki yake ndiyo iliyomsaidia (Isaya 59:16). Bwana, kama Wewe ungehesabu maovu, Ee Bwana, nani angesimama? Lakini kwako kuna msamaha, ili Wewe uogopwe (Zaburi.130:3,4). Ndiyo rehema na msamaha ni kwa Bwana Mungu wetu, ingawa tumemwasi (Danieli 9:9). Katika Wewe huyo, kwa damu yako, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yako (Waefeso.1:7). Tunajinyenyekeza mbele zako, na tunakuomba utuongoze katika hukumu na utufundishe njia zako (Zaburi.25:9). Utusaidie tusiishi kwa kufuata mambo ya mwili, bali kwa kuyafisha matendo ya mwili kwa Roho (Warumi 8:13). Tunataka kujifunza kuenenda katika Roho ili tusiweze kuzitimiza kamwe tamaa za mwili. Tunda la Roho na likawe dhahiri katika kanisa – Upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi (Wagalatia.5:16-26). Utusaidie tuwe na mwenendo mzuri kati ya Mataifa ili, iwapo huwasingizia kuwa watenda mabaya, wayatazamapo matendo yenu mazuri, wamtukuze Mungu siku ya kujiliwa. (1Petro.2:11-12). Utusamehe kwa kuwa na nia ya mwili, na utusaidie kuyafikiria mambo ya roho ilituweze kukupendeza wewe (Warumi.8:5-8). Tuna kusihi utugeuze kwa kufanya upya nia zetu, kupitia neno lako, ili tusiifuatishe namna ya dunia hii. Tupate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu (Warumi.12:2). Ufalme wako na uje, thibitisha haki yako na hukumu kwa Mataifa ya ulimwengu (Luke 11:12; Isaya.9:7).

Saa ya 8: Saa 1:00 – 2:00 Asubuhi

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea usomaji wa Biblia)

Usomaji wa Biblia: Saa ya pili ya kusoma Zaburi - angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Nguvu ya Maombi ya pamoja

Baba, Mwana na Roho Mtakatiju, Mungu mmoja. Tunakiri kwamba kuna Mwili Mmoja, Roho Mmoja, Imani Mmoja, Ubatizo Mmoja, Mungu Mmoja nawe ni Baba wa Wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote. (Waefeso.4:4-6). Tunakuomba wewe, Mungu mwenye saburi na faraja utujalie Kanisa katika mataifa ya dunia kunai mamoja sisi kwa sisi tunapokutafua uso wako, ili kwa moyo mmoja na kwa kinywa kimoja tupate kumtukuza Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo. Tusaidie tuweze kukaribishana sis kwa sisi, kama naye Kristo alivyotukaribisha, ili Mungu atukuzwe (Warumi.15:1-7).

Tunakiri kwamba mwenendo wetu hapa zamani haukuwa kama ipasavyo Injili ya Kristo, , lakini sasa tunatamani kusimama imara katika roho moja, kwa moyo mmoja tukiishindania imani ya Injili (Wafilipi.1:27). Tunasikitika kwamba tumeangalia mambo yetu wenyewe hatukuangalia mambo ya wengine, lakini sasa tunakiri ubinafsi wetu na majivuno, na kwakunia manyonge tunajinyenyekeza mbele zako tukiomba msaada wako ilituweze kuwahesabu wenzetu kuwa bora kuliko nafsi zetu (Wafilipi.2:2-4). Kama tujavyo kuomba pamoja tupe kunai mamoja, wenye kuhurumiana, wenye kupendana kama ndugu, wasikitikivu, wanyenyekevu; watu wasiolipa baya kwa baya, au laumu ka laumu; bali wenye kubariki; kwa sababu hayo ndiyo tuliyoitiwa ili turithi baraka (1 Petro.3:8-9). Hatuta kuwa watu wa kujivunia akili, na hatutania yaliyo makuu, lakini kukubali kushughulishwa na mambo manyonge (Warumi.12:16). Utusaidie kuchukuliana katika upendo, haitupasi kujipendeza wenyewe, kama Kristo naye hakujipendeza mwenyewe. (Warumi.15:1-3), na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani (Waefeso.4:2-3), na haribu tafadhari umoja wowote usio mtakatifu unaovuruga maombi yetu (Ufunuo.17:13).

Ahsante kwa kutupa mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji, na walimu kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hat

tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikamanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo (Waefeso.4:11-16). Yesu alituahidi kwamba tukifanya maombi pamoja, na kupatana katika lile tunaloomba, kwamba wewe, Baba yetu uliye mbinguni, utatupa tunayoomba na kwamba utakuwa kati yetu (Mathayo.18:19-20).

Tutie moyo kudumu katika kukungoja ahadi zako ilitusi kate tamaa (Luka 18:1). Ahsante ingawa tu dhaifu na hatujui kuomba, Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua, Wewe uchunguzaye mioyo, tafadhali sikia maombi yetu (Warumi.8:25-27).

Basi Mungu wa tumaini na atujaze sis furaha yote na amani katika kuamini tupate kuzidi sana kuwa na tumaini, katika nguvu za Roho Mtakatifu.

Saa ya 9: Saa 2:00-3:00 Asubuhi

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea kusoma Biblia)

Usomaji wa Biblia: Saa ya Tatu ya kusoma Zaburi - angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Kuachiliwa kwa Roho wa Mungu

Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, tunakushukuru kwamba tunaweza kuishi katika maongozi na wakati ambapo Roho wako Mtakatifu ametolewa kufundisha, kuongoza na kutufariji (Yohana 14:26). Tunakushukuru kwamba katika siku ya Pentecoste, kama miaka 2000 iliyopita, kanisa lilizaliwa kupitia ubatizo wa moto, ulipotimiza ahadi yako na kuachilia Roho yako juu ya wote wenye mwili (Yoeli 2:28-32; Matendo 2:1-4; 17-21; Mathayo.3:11). Tunakushukuru kwamba kuachiliwa kwa Roho Mtakatifu inathibitisha kwamba ulikubali toleo Yesu alilolifanya kutupatanisha na Wewe, na ametukuzwa mkono wako wa kuume (Matendo 2:33). Tunakushukuru kwamba umelipa kanisa Uwezo kupitia Roho Mtakatifu kutangaza Injili ya Yesu Kristo kwa Mataifa yote na sisi ni mashahidi wa uaminifu wako, wakati ambapo mataifa mengi ya ulimwengu yatakapo ungana katika siku ya maombezi ya ulimwengu (Matendo 1:8). Tunashukuru kwa karama za Roho Mtakatifu ambaye anashuhudia nia yako kwa watu wote kulijua neno lako (Mithali 1:23; 1 Wakorintho.12:1-30; Waebrania.2:4).

Tunakushukuru kwamba kupitia Roho Mtakatifu, tumepokea Roho ya kufanywa wana (Warumi.8:15; Wagalatial.4:6) twaweza kukujua (Waefeso.1:17) na kukuita “Abba Baba”, na kwamba hutatuacha sisi yatima bali umetuma msaidizi (Yohana 14:16,18; Yohana 15:26). Tunakushukuru Wewe kwamba tumetiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu. Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi wa milki yake, na kupitia Yeye tuna takaswa (Waefeso.1:13,14; 2 Wathesolanike.2:13; 1 Petro.1:2). Tumefanyika hekalu la Roho Mtakatifu na tu mali yake (1 Wakorintho.6:19). Tunakushukuru kwa kutuosha, kutusafisha na kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wako, ili katika kweli tufanyike maskani yako (Tito 3:5; Waefeso.3:16). Tafadhali utusamehe mara nyingi tulivyo mkwaza na kumhuzunisha Roho Mtakatifu, au kwa kutaa kutii njia zako na tumempinga Roho wako (Waefeso.4:30; 1 Wathesolanike.5:19; Matendo 5:9). Tulinde dhidi ya kuongea kinyume, kuasi au kusema uongo kwa Roho Mtakatifu ili usitugeuke na kufanyika adui yetu na kupigana nasi (Mathayo.12:32; Matendo 5:3; Isaya.63:10,11).

Roho wako anatupatia hekima na ujasiri wa kushirikisha Neno lako kwa watu wote, hata kwa walio katika Mamlaka (Danieli.4:9; 5:11; Matendo 4:18). Tupatie

ujasiri zaidi kwamba hata kama tunateswa tutasema kweli bila kukaa kimya kuhusu upendo wako natumaini tulilonalo mioyoni mwetu (Matendo 4:31; Warumi.5:5). Utusaidie kumbuka kwamba Roho wako atatupa maneno sahihi wakati ambapo imani yetu inapotishiwa (Marko 3:11; Luka 12:11-12). Tupe hekima ilitujue namna ya kuwahudumia wale wenye mahitaji (Matendo 6:3). Maana Wewe Mungu hukutupa Roho wa woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi (2 Timotheo.1:7). Tunda la Roho lidhihirike ndani na katika maisha yetu (Wagalatia.5:22-23).

Nafsi zetu zinakuonea shauku, Ee Mungu, kama ardhi yenye kiu na kavu tunatamani Wewe uachilie Roho wako tena (Zaburi.63:1; Isaya.44:3). Zitume nyakati za kuburudishwa na utuhuishe Ee Bwana (Matendo 3:19; Zaburi.85:6). Yesu alitualika: “Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe. Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake.” Tafadhali achia maji haya yaliyo hai yakate kiu yetu na mito ya maji ikatoke kutoa uhai kwa mataifa (Yohana 7:37-39). Roho Mtakatifu akatutume na akatujaze na tumaini kwa nguvu zake (Matendo 13:4; Warumi15:13).

Karibu, Roho Mtakatifu na uhakikishie ulimwengu kwa habari ya dhambi na haki na hukumu (Yohana16:7-8). Na kanisa Lako likajengwe, likiendelea na kuongezeka katika kicho cha Bwana, na faraja ya Roho Mtakatifu (Matendo 9:31).

Saa ya 10: 3:00 – 4:00 Asubuhi

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea na kusoma Biblia)

Usomaji wa Biblia: Soma toka Mwanzo hadi Ufunuo - angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Sauti ya Mungu

Baba yetu wa Mbinguni, tunaungana na wana wa Mungu na kusema mpeni BWANA utukufu na nguvu; mpeni Bwana utukufu wa Jina lake; Mwabuduni Bwana kwa uzuri wa utakatifu wake. Sauti ya Bwana i juu ya maji; Mungu wa utukufu alipiga radi; Bwana yu juu ya maji mengi. Sauti ya Bwana ina nguvu; sauti ya Bwana ina adhama; sauti ya Bwana yaivunja mierezi; naam, Bwana aivunja vunja mierezi ya Lebanoni. Sauti ya Bwana yaipasua miali ya moto; sauti ya Bwana yalitetemesha jangwa (kiza juu ya Mataifa); Sauti ya Bwana yawazalisha ayala. Na kuifichua misitu; na ndani ya hekalu lake (mioyo ya kanisa) wanasema wote: “UTUKUFU!” (Zaburi 29:1-9)

Baba ulisema: “Iwe nuru!” na ikawa nuru… (Mwanzo.1:3). Katika giza la ulimwengu huu, ulimtuma mwanao; naye Neno alifanyika mwili! (Yohana 1:1-14) na ikwa nuru…! Ahsante kwa kumtuma mwanao, ili tuweze kuiona nuru, na kuwa na matumaini mioyoni mwetu (Waefeso.1:18). Sauti yako toka mbinguni ilituamuru tumsikie Mwanao (Marko 9:7). Yesu alisema kwamba Yeye ni mchungaji mwema, na kondoo zake wote wataisikia sauti Yake (Yohana 10:3-5; 14-16). Utusaidie kuitambua kweli kwenye uongo na kuijua sauti yako kwa hakika (Yohana 18:37) na tutakapoisikia sauti yako, utusaidie tusifanye migumu mioyo yetu na kukuasi. Ututakase na utusafishe ili mioyo yetu isiwe miovu isiyoamini, lakini tuwe na imani kwako (Waebrania 3:7-15).

Fungua masikio yetu tusikie na kukutii, maana ulisema: “kutii ni bora kuliko dhabihu…” (Zaburi. 40:6; 1 Samweli.15:22-24) Tunakuomba utusamehe kwa nyakati zile tuliposikia sauti yako lakini hatukuzingatia na hatukutii na hatukufanya uliyotuambia tuyafanye. Tuwezeshe tena kuisikia sauti yako kadri unapotuongoza kukufuata (Isaya.30:21).

Tunaomba kwamba Mataifa waisikie sauti yako, hata kama Mataifa hayo yameghadhibika na falme zimetaharuki (Zaburi.46:6). Uwawezeshe wale wasiokujua au kutojali kukutii Wewe, wauone uweza wako na wainame mbele zako (Kutoka.5:2). Tupe maneno Yako ili tuwe sauti yako kusema na serikali na viongozi ili tuwasaidie waenende katika njia zako (Marko 3:11). Utusaidie kukukaribia kupokea jumbe zako unazotaka kuzitoa kupitia kanisa lako (Kum la

Torati.5:25-27). Tupe pia uwezo wa kusema na kutafsiri injili katika lughambalimbali za watu (Matendo 2:11).

Ni wakati wa kuamshwa kwa bibi arusi. Kanisa na lisikie sauti ya Bwana arusi na lifungue moyo wake Kwako (Wimbo ulio Bora.2:8; 5:2). Tuwezeshe kukukaribia karibu sana tuweze kujua haja za moyo wako na tuweze kujitoa katika utumishi wako (Isaya.6:8). Na muda utakapofika kwa wafu kusikia sauti yako, tutanyakuliwa katika ufufuo wako wa uzima (Yohana 5:25-29), na kuwa nawe milele.

Saa ya 11: 4:00 – 5:00 Asubuhi

(Omba maombi lako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea na usomaji wa Biblia)

Usomaji wa Biblia: Soma toka Mwanzo hadi Ufunuo - angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Mahusiano ya kanisa

Bwana Yesu Kristo, Wewe ni kichwa ncha mwili, yaani kanisa; nawe ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba uwe mtangulizi katika yote. Katika Wewe ilimpendeza Baba utilimilifu wote ukae, na kwa Wewe kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yako, ukiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wako (Wakolosai.1:18-20).

Tunakiri kama kanisa tumeshindwa kuutambua mwili wako kwa uhakika lakini tumenia makuu kupita ilivyotupasa kunia, tukisahau kwamba ni mwili mmoja ukiwa na viungo mbali mbali wala viungo vyote havitendi kazi moja, bali kila kiungo kwa mwenzake (Warumi.12:3-5). Tunakiri kwamba tumejivuna bure kwa akili zetu za mwili na kama mwili tumepoteza mawasiliano na Wewe uliye kichwa, na mwili umedhurika na kuachamanika na kushindwa kukua kufikia utu uzima (Wakolosai.2:18-19). Tumeendelea kuumana na kulana na baadhi yetu wameangamizwa kwa kutowaonyesha upendo wetu (Wagalatia.5:14-15). Tafadhali utusamehe na urejeshe mahusiano yetu. Umeuungamanisha mwili ili kusiwe na faraka katika mwili, bali viungo vitunzane kila kiungo na mwenziwe na kiungo kimoja kikiumia viungo vyote huumia, na kiungo kikitukuzwa, viungo vyote hufurahi pamoja nacho (1 Wakorintho.12:24-27). Na tuwe na umoja kama Wewe na Baba mlivyo wamoja. Tunaomba kwamba maombi yako yajibiwe na Baba kwamba Mungu atulinde kwa uwezo ulio katika Jina lake, Jina ulilopewa Wewe, ili kwamba umoja wetu uweze kudhihirishwa katika upendo tunaouonyesha kati yetu sisi kwa sisi (Yohana 17:11), Ni kupitia upendo huu kwamba ulimwengu utatambua kwamba sisi tu wako (Yohana 13:25).

Bwana Yesu Kristo, utusaidie kuuvua kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani, unaoharibika kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya; na tufanywe upya katika roho ya nia zetu, tukavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli, ili tuishi pamoja kama viungo katika mwili mmoja (Waefeso.4:22-25). Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwetu (Wakolosai.3:15), ili kwamba tunapofunga na kuomba na kujinyenyekesha, na kuutafuta uso wako uweze kutujibu na uje kuiponya nchi yetu (Isaya.58:3-4; 2 Nyakati.7:14).

Siri uliyo ifunua kwa kanisa ni kwamba kupitia injili sisi Mataifa tumekuwa warithi pamoja na Israeli, na wa mwili mmoja, na washiriki pamoja katika ahadi yake iliyo katika Kristo Yesu (Waefeso.3:6). Tunapoomba pamoja kama Mataifa ya ulimwengu, turejeshe, kanisa lako katika makusudi yako uliyoyakusudia hata kabla hujatuumba (Waefeso.2:15; Waefeso.3:10,11). Tunapopokeana katika umoja, Jina lako litukuzwe (Warumi.15:7).

Tazama, jinsi ilivyo vyema, na kupendeza, ndugu wake pamoja, kwa umoja. Ni kama mafuta mazuri kichwani, yashukayo ndevuni, ndevu za Haruni, yashukayo mpaka upindo wa mavazi yake, maana ndiko Bwana alikoamuru baraka, naam, uzima hata milele! (Zaburi.133:1-3) Na kanisa lako lipate ujuzi wa maisha haya yanayotoka kutoka kichwani hata mwilini, wote tukiungana katika umoja. Amina.

Saa ya 12: 5:00 – 6:00 Mchana

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea na usomaji wa biblia)

Usomaji wa Biblia: Soma toka Mwanzo hadi Ufunuo - angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Damu ya Yesu Kristo

Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai, wala hapakuwa na mtu mbinguni, wala juu ya nchi, wala chini ya nchi, aliyeweza kukifungua hicho kitabu, wala kukitazama, isipo kuwa Wewe. Pamoja na wale wenye uhai wa nne na wale wazee ishirini na wanne tunaanguka mbele zako tukisema: “Wastahili Wewe kukitwaa kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa.” (Ufunuo.5:3,9)

Mungu Baba, ahsante kwa damu iliyofanyika sadaka ya nafsi zetu pale madhabahuni (Walawi.17:11) na ile damu ya mwana kondoo ikawa ishara ya pasaka ulipowakomboa watu wako kutoka Misri (Kutoka.12:13). Tokea hapo ulitaka damu ya ile sadaka ya dhambi ya kufanya upatanisho (Kutoka.30:10; Kumbukumbu.21:8). Na katika torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo (Waebrania.9:22); Lakini tumekuja kwa Yesu mjumbe wa agano jipya, na damu ya kunyunyizwa, inenayo mema kuliko ile ya Habili (Waebrania.12:24). Ahsante kwa kuonyesha pendo lako wewe mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi (Warumi.5:8). Ndiyo, umekwisha kumweka awe upatanisho na kwa damu Yake ulionyesha haki yako, kwa kuwa Yesu alikuja kama kuhani Mkuu na kwa damu yake aliingia patakatifu pa patakatifu mara moja kwa ajili ya wote na kutupatia ukombozi wa milele (Warumi.3:25; Waebrania.9:11-12). Kwa damu ya thamani ya Yesu Kristo, kama mwana kondoo asiye na mawaa wala madoa, umetukomboa na kutusamehe dhambi zetu sawasawa na utajiri wa neema yako (1 Petro.1:18-19; Waefeso.1:7; Col.1:14). Hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu, tumeletwa karibu katika kiti chako cha enzi kwa damu yake Yesu (Waefeso.2:5;13). Ni kwa kupitia damu ya Yesu tumehesabiwa haki na kupatanishwa nawe, Mungu wetu wa mbinguni (Warumi.5:9; Wakolosai.1:20).

Bwana Yesu Kristo, ahsante kwa kujitoa nafsi yako kwa Mungu kupitia Roho wa milele, kama sadaka isiyo na mawaa na hivyo kutununua, kanisa la Mungu, kwa damu yako (Matendo 20:28). Ni damu yako inayosafisha dhamira zetu na matendo mafu, tupate kumwabudu Mungu aliye hai (Waebrania.9:14). Ulitupenda na kutusafisha dhambi zetu kwa damu yako sasa tumesafishwa

dhambi zote (Ufunuo.1:5; 1 Yohana1:7) na umetutakasa katika Roho kwa damu yako (Waebrania.13:12; 1 Petro.1:2). Ni kwa kupitia damu yako tunamshinda shetani (Ufunuo.12:11).

Usiku kabla ya kujitoa kama sadaka ya kuteketezwa, ulichukua kikombe na kusema: “Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; uliyomwagwa kwa wengi kwa ajili ya ondoleo la dhambi.” (Luka 22:20; 1 Wakorintho.11:25). Pia ulisema yeye alaye mwili wangu na anywaye damu yangu ana uzima wa milele, na mwili wako ni chakula cha kweli, na damu yako ni kinywaji cha kweli (Yohana 6:53-56). Kikombe kile cha baraka tukibarikicho, je! Si ushirika wa damu ya Kristo? Mkate ule tuumegao, si ushirika wa mwili wa Kristo? (1 Wakorintho.10:16). Ahsante kwamba tunaweza kushiriki agano hili jipya katika damu Yako ulilolifanya na Mungu Baba tunaposheherekea ushirika. Ahsante kwa njia ile uliyotuanzia iliyo mpya, iliyo hai, ipitayo pazia yaani mwili wake, na kwamba tunao ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu (Waebrania.10:19-20).

Sasa tunaomba, Ee Mungu wa amani, uliyemfufua Bwana wetu Yesu kutoka mauti, mchungaji mkuu wa kondoo, utukamilishe katika kila kazi njema kupitia damu ya agano la milele, Yeye Bwana wetu Yesu, atufanye sisi kuwa wakamilifu katika kila tendo jema, tupate kuyafanya mapenzi yake; naye akifanya ndani yetu lipendezalo mbele zake, kwa Yesu Kristo; utukufu una Yeye milele na milele. Amina. (Waebrania.13:20-21).

Saa ya 13: Saa 6:00 -7:00 Mchana

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea na usomaji wa biblia)

Usomaji wa Biblia: Soma toka Mwanzo hadi Ufunuo - angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Kibali katika kiti cha enzi

Baba, kwa sababu ya mwaliko wako tunakaribia kiti chako cha neema kwa ujasiri, ili tupate rehema na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji (Waebrania 4:16). Ulituahidi kwamba tukuite, nawe utatuitikia, nawe utatuonyesha mambo makubwa, magumu tusiyoyajua (Yeremia.33:3). Ulipokufa msalabani maneno yako ya mwisho yalikuwa: “Imekwisha”, baada ya hapo pazia lilipasuka na sasa tuna kibari cha kuingia moja kwa moja katika kiti chako (Yohana19:30). Basi sasa, tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu pa patakatifu kwa damu ya Yesu, kwa njia ile mpya aliyotuanzia, iliyo hai, ipitayo katika pazia yaani mwili wake; na kuwa na kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu na tukaribie wenye moyo wa kweli; kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyizwa mioyo tuache dhamiri mbaya; tumeoshwa miili kwa maji safi (Waebrania.10:19-22).

Baba, kwa ujasiri tunakaribia katika kiti chako kwa sababu ya Yesu kutuombea. Kwa sababu Kristo hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu (Waebrania.9:24). Tunaamini katika ahadi zako nyingi, maana ahadi zote za Mungu zilizopo katika yeye ni Ndiyo; tena kwa hiyo katika yeye ni Amini; Mungu apate kutukuzwa kwa sisi (2 Wakorintho.1:20). Bwana Yesu, Uliahidi: “Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa.” (Mathayo.7:7-8) Imani yetu katika ahadi zako imejengwa katika tabia yako. Neno lako linatufundisha kwamba Mungu si mtu hata aseme uongo; wala si mwanadamu, ajute, iwapo amesema, hatalitenda? Iwapo amenena, hatalifikiliza? (Hesabu.23:19) Bwana Yesu, tumaini letu na faraja yetu ipo katika Jina lako kwa sababu ulituahidi kwamba utatupa kila tuombalo katika Jina lako, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Ulituahidi kwamba tukikuomba lo lote katika Jina lako utalifanya! (Yohana 14:13-14).

Tunakuomba kwa sababu ya agano lako nasi ambapo ulitamka kwamba utakuwa baba kwetu, nasi tutakuwa kwako wana wa kiume na wa kike (2 Wakorintho.6:18; Waebrania.8:10) Katika neno lako Mungu, ukitaka kuonyesha zaidi sana wairithio ile ahadi, jinsi mashauri yako yasivyoweza kubadilika, ulitia kiapo katikati; (Waebrania.6:17). Umetuumba tuwe wawakilishi wako hapa

duniani na kutufanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu, ili tukutumikie kupitia kuabudu kwetu, na kushikilia na kukukumbusha dhabihu yote iliyo kamili ya Yesu kadri tunapotimiza wajibu wetu wa kikuhani mbele ya kiti chako (Ufunuo.1:6). Tunapokaribia kiti chako ili kuombea ulimwengu, tunashikilia ahadi ambayo tutaipokea toka kwako, neema juu ya neema. (Yohana 1:16).

Baba, hakuna jambo gumu mbele zako (Mathayo.17:20) kwa maana hakuna upendeleo kwa Mungu (Warumi.2:11). Hivyo tunakaribia kiti cha neema kwa ujasiri na uhakika wa kwamba utatusikia na tutapokea msaada wako (Waebrania 4:16).

Saa ya 14: 7:00 – 8:00 Mchana

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea na usomaji wa Biblia)

Usomaji wa Biblia: Soma toka Mwanzo hadi Ufunuo - angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Makusudi ya Mungu - Kanisa

Bwana Yesu Kristo, Kichwa cha kanisa, utaliimarisha kanisa lako kupitia Injili na kutangazwa kwa Yesu Kristo msulubiwa, sawasawa na ufunuo wa ile siri iliyositirika tangu zamani za milele. Ikadhihirishwa wakati huu kwa maandiko, ikajulikana na mataifa yote kama alivyoamuru Mungu wa milele, ili waitii imani (Warumi.16:25-27). Baba tunakushukuru kwa neema uliyotupa katika Kristo Yesu. Kwa kuwa katika kila jambo tulitajirika katika yeye, katika maneno yote na maarifa. Kama ushuda wa Kristo ulivyothibitika kwetu, tukikutazamia sana kufunuliwa kwake Bwana wetu Yesu Kristo hata tusipungukiwe na karama yo yote katika kufanya kazi yako ututhibitishe hata mwisho, ili tulilaumiwe siku ile ya Bwana wetu Yesu Kristo (1 Wakorintho.1:4-8).

Baba, katika hali ya shukurani na sala ninaomba tuongezewe upendo na imani katika kanisa. Wewe, Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, utupe sisi roho ya hekima na ya ufunuo katika kukujua Wewe; macho ya mioyo yetu yatiwe nuru, tujue tumaini la wito wako jinsi lilivyo; na ubora wa ukuu wa uweza wako ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wako; uliotenda katika Kristo ulipomfufua katika wafu, ukamweka mkono wako wa kuume katika ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; ukavitia vitu vyote chini ya miguu yake, ukamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wako, ukamilifu wako anayekamilika kwa vyote katika vyote (Waefeso.1:15-23).

Tunapiga magoti mbele zako Baba ambaye katika Jina lako ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa, utujalie, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wako, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wako, katika utu wa ndani. Kristo akae mioyoni mwetu katika imani tukiwa na shina na msingi katika upendo; ili tupate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, tupate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu. Basi utukuzwe Wewe uwezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu; naam utukuzwe katika kanisa na

katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele. Amina (Waefeso 3:14-21).

Lirejeshe kanisa kama nyumba ya maombi ili kanisa liweze kujitoa tena katika kukesha katika kuomba huku na shukrani (Wakolosai.4:2). Usiku na mchana tunapoomba kwa juhudi ili uweze kutengeneza mapungufu ya imani yetu, Bwana utuongeze na kutuzidisha katika upendo, sisi kwa sisi, na kwa watu wote, upate kuifanya imara mioyo yetu iwe bila lawama katika utakatifu mbele zako Mungu, Baba yetu, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu pamoja na watakatifu wote (1 Wathesalonike.3:9-13). Baba kwa ujasiri tunaomba kwamba Wewe uliyeanza kazi njema mioyoni mwetu utaimaliza hata siku ya Kristo Yesu. Tunaposhiriki neema yako, pPendo letu lizidi kuwa jingi sana, katika hekima na ufahamu wote; tupate kuyakubali yaliyo mema; ili tupate kuwa na mioyo safi, bila kosa, mpaka siku ya Kristo; hali tumejazwa matunda ya haki, kwa njia ya Yesu Kristo, kwa utukufu na sifa ya Mungu. (Wafilipi.1:6-11).

Saa ya 15: Saa 8:00 – 9:00 Mchana

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea na usomaji wa Biblia)

Usomaji wa Biblia: Soma toka Mwanzo hadi Ufunuo - angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Makusudi ya Mungu kwa familia na watoto

Baba wa Bwana na Mwokozi wetu Yesu, tunapiga magoti mbele zako ambaye kwa jina lako ubaba wote wa mbinguni na duniani unaitwa (Waefeso.3:14,15). Sisi, kama jamaa za watu tunakupa Bwana utukufu na nguvu, tunasema katika mataifa: “Bwana ametamalaki! Atawahukumu watu kwa adili.” (Zaburi.96:7-10) Ahadi yako kwa Ibrahimu ni kwamba kupitia yeye jamaa zote za dunia watabarikiwa (Mwanzo.12:3). Hakika umetubariki kwa kumtuma Mwanao kutufia msalabani ili kutupatanisha na Wewe (Wakolosai.1:20).

Kwa kuwa familia zote mwanzo wake ni kwako, tunakuomba ulete uponyaji na urejesho katika familia za dunia. Tunakubali na kukiri kwamba maumivu mengi ambayo familia zinapitia ni kwa sababu ya njia zetu za uovu. Tunakiri kwamba hatujaishi kutokana na viwango vyako katika ndoa, katika kulea watoto na kuwatunza wale walio yatima (Isaya.1:23). Tumedharau amri zako kwamba waume wawapende wake zao, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, na wake wawatii waume zao kama kumtii Bwana wetu (Waefeso.5:22-33; 1 Petro.3:7). Kupitia damu yako twapatanishwa sisi kwa sisi (2 Wakorintho.5:18; 1Wakorintho.7:11). Tusaidie kuheshimu miili yetu na kuwajibika kwa wale uliotupa (1Wakorintho.7:2-5). Na ndoa zetu ziwe kielelezo cha uhusiano wako na kanisa (Waefeso.5:22-33), ili upate utukufu.

Tunakiri pia kwamba kama watoto hatuwatii wazazi wetu na hatuwaheshimu kama ulivyotuamuru tufanye (2Timotheo. 3:2; Kutoka. 20:12). Kama wababa na wamama hatujaweka mifano kwa watoto wetu kwa maisha ya kimungu. Tumewasababishia kujikwa na kuwachokoza wakakasirika, na hatujakupa Wewe utukufu kwa kuwaambia kuhusu Wewe, hivyo wakawa waasi na wasio waaminifu kwako (Waefeso.6:4-6; Zaburi.78:4-8). Tunahitaji kusafishwa nawe, na uponyaji, tafadhalil njoo na uoshe familia zetu na neno lako (Waefeso.5:26). Wewe ni Baba wa yatima na mwamuzi wa wajane; unaona taabu na huzuni tuliyojisababishia kwa sababu ya njia zetu mbaya. Tafadhali leta hukumu kwetu, uwaokoe watoto wetu na mvunje vipande vipande mdhalimu (Zaburi.68:5; Zaburi.10:14). Na watoto wetu na wawe uruthi wa Bwana na wakalete furaha mioyoni mwetu (Zaburi.127:3-5; Zaburi.72:4). Bwana Yesu, uliwaita watoto wadogo waje kwako, na kuahidi ufalme wa Mungu ni wao (Marko 10:14).

Mwaliko huu na uwafikie mamilioni ya watoto walioachwa na kupotea bila kwa na familia. Na kizazi chetu kikugeukie na kikalete utukufu katika Jina lako na uturehemu ili tuwaeleze watu wa kizazi hiki nguvu zako na kila atakayekuja uweza wako (Zaburi.71:18), na watu watakaoumbwa watamsifu Bwana (Zaburi.102:18).

Na sasa tunakuita, Baba, uliyetuwezesha kuzaliwa katika familia yako, liwezeshe kanisa lako tena kurejeshwa katika makusudi yako uliyotuumbia, kuenenda katika upendo, na tukawe harufu ya manukato, sadaka na dhabihu kwa Mungu (Waefeso.5:1,2). Tunakushukuru kwamba kupitia Roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, “Aba, yaani, Baba” (Warumi.8:15)

Saa ya 16: Saa 9:00 – 10:00 Alasiri

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea na usomaji wa Biblia)

Usomaji wa Biblia: Soma toka Mwanzo hadi Ufunuo - angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili: Uponyaji wa Kristo
Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA, wala usizisahau fadhili zake zote. Akusamehe maovu yako yote, akuponya magonjwa yako yote! (Zaburi.103:2-3).

Yahweh-Rapha, Wewe ni Mungu, Mponya wetu (Kutoka.15:26). Umetupa Mwana wako, Yesu Kristo kuyachukua masikitiko yetu, na amejitwika huzuni zetu. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Na Bwana umeweka juu yake maovu yetu sisi sote. Lakini Bwana aliridhika kumchubua; umemhuzunisha; utakapofanya nafsi yake kuwa dhabihu kwa dhambi. Kwa sababu alimwaga nafsi yake hata kufa, na kuwaombea wakosaji (Isaya.53:1-12). Ulimtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu, kuhubiri habari njema ya ufalme, na kuponya ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu, hata kuwaponya na mateso ya mapepo (Mathayo. 4:23-24; Matendo 10:38). Jua la haki litawazukia, lenye kuponya katika mbawa zake (Malaki.4:2).

Bwana Yesu Kristo, tunauhitaji wa mguso wa uponyaji wako. Utuponye roho zetu maana tumekutenda dhambi (Zaburi.41:4). Ponya waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka wa dhambi uhuru wao, na hao waliofungwa na madawa, vifungo binafsi, mioyo miovu na ngome za kiroho kufunguliwa kwao (Isaya 61:1).

Bwana Yesu, angalia sasa mioyo yetu, na utuchague, watumishi wako, tuwe na uweza wa kuponya magonjwa na kutoa mapepo, nyoosha mkono wako kwa Roho Mtakatifu kuponya, ishara na maajabu vifanyike kwa Jina la Mtumishi wako mtakatifu Yesu. Tujaze upya kwa Roho wako ili kwa ujasiri tuweze kuufikia ulimwengu ulio na mahitaji (Matendo 4:29-31).

Umetuahidi kwamba ikiwa sisi watu wako, tulioitwa kwa jina lako, tutajinyenyekesha, na kuomba, na kukutafuta uso, na kuziacha njia zetu mbaya; basi, utasikia toka mbinguni, na kutusamehe dhambi zetu, na kuiponya nchi yetu. (2Nyakati.7:14). Mataifa yetu yanauhitaji wa kuponywa. Timiza ahadi yako kwa kuleta uponyaji, tunapojinyenyekesha mbele yako, tukiungana katika maombi ya pamoja kuutafuta uso wako, na kuziacha njia zetu mbaya. Tupe mioyo mipya na roho mpya na utoe mioyo ya jiwe iliomo ndani ya miili yetu na utupe mioyo ya

nyama. Tia roho yako ndani yetu na kutuendesha katika sheria zako (Ezekieli.36:26-29). Uoshe uchafu wetu na utusafishe kwa Roho yako ya hukumu na kwa roho ya kuteketeza (Isaya.4:4).

Wewe ambaye ni mtoa uzima, umetupatia uzima. Katika kiti chako cha enzi kuna mti wa uzima, na majani ya mti huoni ya kuwaponya mataifa (Ufunuo.22:2). Turuhusu kuingia katika uwepo wako kupokea uzima huo kutoka kwako. Tunakuabudu. Wewe ndiye Njia, na Kweli, na Uzima (Yohana 14:6).

Saa ya 17: Saa10:00 – 11:00 Alasiri

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea na usomaji wa Biblia)

Usomaji wa Biblia: Soma toka Mwanzo hadi Ufunuo - angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Baraka za Kristo

Mwana kondoo wa Munguj. Mwokozi wangu, wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kabila na lugha na jamaa na taifa na ukatufanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki juu ya nchi! (Ufunuo.5:9) Astahili Mwana-kondoo aliyechinjwa, kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka! (Ufunuo. 5:12)

Bwana Yesu Kristo, ulikuwa una namna ya Mungu, nawe hukuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali ulijifanya kuwa huna utukufu, ukatwaa namna ya utumwa, ukawa una mfano wa wanadamu; tena, ulipoonekana una umbo kama mwanadamu, ulijinyenyekeza ukawa mtii hata mauti, naam mauti ya msalaba. Kwa hiyo tena Mungu alikwadhimisha mno, akakukirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba. Nina piga magoti na kukiri kwamba Yesu Kristo ni Bwana wa maisha yangu (Wafilipi.2:5-11).

Bwana Yesu Kristo, Wewe ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote; Kwa kuwa katika Wewe vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni viti vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yako, na kwa ajili yako. Nawe umekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikamana katika Wewe. Nawe ndiwe kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; nawe ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba uwe mtangulizi katika yote. Kwa kuwa katika Wewe ilipendeza utumilifu wote ukae; na kwa Wewe kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yako, ukiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wako; kwa Wewe, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni, tukiwa na amani kupitia damu ya msalaba wako. Sasa mimi miliokuwa hapo kwanza nimefarikishwa, tena adui katika nia yangu, kwa matendo yangu mabaya, amenipatanisha; katika mwili wa nyama, kwa kufa kwake, ili anilete mimi mbele zake, mtakatifu, niseye na mawaa wala lawama mbele za Mungu (Wakolosai.1:15-23). Nakushukuru kwamba nimekamilishwa kwako. Nilikufa pamoja na Wewe uliposulubiwa, na nikazikwa na nikafufuliwa pamoja na Wewe

katika imani katika kazi ya Mungu, Aliyekufufua Wewe katika wafu. Mimi niliyekuwa nimekufa kwa sababu ya makosa yangu na kutokutahiriwa kwa mwili wangu, alinifanya hai pamoja naye, akiisha kunisamehe makosa yote akiisha kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu yake, iliyokuwa na uadui kwetu; akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea msalabani (Wakolosai.2: 9-14).

Bwana Yesu, tunakushukuru kwa agano jipya liliondikwa katika damu Yako (Mathayo.26: 26-29; 1Wakorintho.11: 23-26); Kwa masamaha ya dhambi kupitia damu yako na kwamba dhambi haitanitawala mimi sababu sipo chini ya sheria, bali chini ya neema (Warumi.6:14). Ninakushukuru kwamba nimehesabiwa haki kwa damu yako, kama vile sijatenda dhambi, na mashitaka yote ya shetani dhidi yangu yamefutwa na nguvu yake kwangu imevunjwa (Warumi.5:9; Wakolosai.1:13). Nakushukuru kwamba kupitia Jina lako na damu Yako, naweza kumshinda shetani na nguvu zake zote (Ufunuo.12:11). Nakushukuru kwa njia ile uliyotuanzia iliyo mpya, iliyo hai, ipitayo katika pazia yaani, mwili wako (Waebrania.10:20), na kwa sababu ya Agano Jipya katika damu yako, nitakuwa na furaha ya milele katika nyuani mwako (Ufunuo 7:9-17).

Bwana Yesu Kristo, Wewe ni yule aliye katika farasi mweupe, ajaye katika haki kuhukumu na kufanya vita. Wewe unaitwa Neno la Mungu na ni Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana! (Ufunuo.19:11-16) Wewe ni Bwana harusi, ambaye bibi harusi, kanisa lako limejiweka tayari (Ufunuo 19:7). Tunapenda kuungana nawe milelel na milele.

Saa ya 18: Saa 11 – 12 Jioni

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea na usomaji wa Biblia)

Usomaji wa Biblia: Soma toka Mwanzo hadi Ufunuo - angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Mateso na taabu

Bwana Yesu Kristo, umetuita kufuate nyayo zako, hata katika mateso; maana Kristo nawe uliteswa kwa ajili yetu ukatuachia kielelezo, tufuate nyayo zako. Wewe ulipotukanwa, hukurudisha matukano; bali ulijikabidhi kwake yeye ahukumuye kwa haki (1Petro.2:21-24). Mateso Yako yalikuwa muhimu ili kwamba tupokee masamaha ya dhambi zetu (Luka 24:46-47), na kwa sababu ya utii wako na kukubali kwako kuteswa, tumehesabiwa haki. Ahsante kwa kujitwika huzuni yetu, ulichubuliwa kwa makosa yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yako, na ili tupokee uzima wa milele (Isaya.53:2-12).

Umewaita kuwa heri wale wanaoudhiwa kwa ajili ya haki na umetuahidi thawabu kubwa mbinguni tunapowabariki wale wanaotushutumu na kutuudhi, kwa sababu ya Jina lako (Mathayo.5:10-12). Utusaidie kunia mamoja na Wewe, ili tuweze kuishi katika mapenzi ya Mungu (1Petro. 4:1,19), na kama kunia huku kutasababisha mateso, tuwezeshe, kama ilivykuwa kwa kanisa la Kwanza, kufurahi na kushangilia; kwa sababu tumehesabiwa haki kupitia mateso kwa ajili ya Jina lako (Matendo 5:41; Wafilipi.1:29; 2 Wathesalonike.1:5-6). Utusaidie kuelewa makusudi ya dhiki, kama Paulo alivyotamka kwamba wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa (Warumi.8: 17; 2 Timotheo.3: 12). Utusaidie kusema kama alivyosema Paulo: “Ili nimjue Yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake.” (Wafilipi.3: 10-11) Tufanye tuweze kufurahia kuteswa kwa ajili ya kanisa, ili kwamba utukufu wako udhihirishwe katika sisi (Wakolosai. 1:24; Warumi.8:18), na utusamehe mahali ambapo tuliona aibu kukushuhudia (2Timotheo.1:8).

Tunawaombea wale wanaoudhiwa na kuteswa kwa ajili ya Jina lako, kwamba Wewe mwenyewe utawatengeneza, na kuwathibitisha, na kuwatia nguvu (1 Petro.5:10). Utusaidie wote sisi kusema: “Tukitukanwa twabariki, tukiudhiwa twastahimili; tukisingiziwa twasihi;” (1 Wakorintho 4:12,13) Pande zote twadhikika, bali hatusongwi; twaona shaka, bali hatukati tamaa; twaudhiwa, bali hatuachwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi; sikuzote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika katika miili yetu (2Wakorintho.4:8-10). Tunataka tuingizwe katika orodha ya watu wa imani waliojaribiwa katika dhihaka na mapigo, naam, kwa mafungo, na kwa kutiwa

gerezani; walipigwa kwa mawe, walikatwa kwa misumeno, walijaribiwa, waliuawa kwa upanga; walikuwa wahitaji, waliteswa, wakitendwa mabaya. Na watu hao wote uliwathibitisha kwa sababu ya imani yao (Waebrania.11:36-40). Tujalie watumwa wako kunena Neno lako kwa ujasiri wote tunapoudhiwa na kutishiwa (Matendo 4:29) Tusaidie pia kujifunza utii kupitia mateso yanayotupata (Waebrania.5:8).

Tunawaombea wale wanaolitesa kanisa lako ili kwamba wakutane na Wewe, na kama Paulo wasipingane na Wewe bali waaanze kulitangaza Jina lako na utukufu Wako kati ya watu wao (Matendo 22:4-16; Matendo 5:39).

Tunakiri na kutamka kwamba mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu (Warumi 8:18). Kama tunavyoshiriki mateso ya Kristo, tufurahi; ili na katika ufunuo wa utukufu wake tufurahi kwa shangwe (1 Petro 4:13). Bwana Yesu uyatawale maisha yetu.

Saa ya 19: Saa 12:00 – 1:00 Jioni

Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea na usomaji wa Biblia)

Usomaji wa Biblia: Saa la nne la usomaji wa Zaburi – angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Serikali

Na lihimidiwe Jina la Mungu milele na milele, kwa kuwa hekima na uweza ni wako. Wewe hubadili majira na nyakati; huuzulu wafalme na kuwamilikisha wafalme; huwapa hekima wenye hekima; huwapa wenye ufahamu maarifa. Wewe hufunua mambo ya fumbo na ya siri; huyajua yaliyo gizani, na nuru hukaa kwako (Danieli.2:20-22).

Baba, kwa dua, sala, na maombezi na shukrani tunakuja mbele ya kiti chako cha enzi kwa ajili ya wafalme, serikali yetu na wale wote walio katika mamlaka, ili tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu, Hili ni zuri, nalo lakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu; ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli (1 Timotheo.2:1-4). Mioyo ya viongozi wetu ipo katika mikono yako Bwana; kama mifereji ya maji huugeuza po pote upendapo (Mithali.21:1). Waondoe washauri waovu kutoka katika viongozi wetu wa serikali, rais na maofisa wengine; thibisha serikali yetu katika haki (Mithali.25:5). Na serikali hii ithibitishwe katika kwa hukumu, ili tuweze kuwa na uthabiti katika nchi yetu. Ondoa tamaa katika mioyo yao na uwalinde wasije kuchukua rushwa (Mithali.29:4). Na serikali yetu iweze kuhukumu maskini kwa uaminifu. (Mithali.29:14).

Mwonyeshi Rais, baraza la mawaziri, na viongozi wote wa serikali; mambo yote mazuri unayoyataka kutoka kwao, fanya kazi katika mioyo yao kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Wewe Mungu wetu (Mika.6:8). Hivyo, katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo tunatamka: Na sasa, enyi wafalme, fanyeni akili; enyi waamuzi wa dunia, mwadibiwe. Mtumikieni BWANA kwa kicho, shangilieni kwa kutetemeka (Zaburi 2:10-11). Bwana Mungu, jaza mioyo ya viongozi wetu upendo na uaminifu, ambavyo vitawaweka salama na kwa namna hiyo tuwe na usalama na amani (Mithali.20:8). Tunaomba utume Roho wako Mtakatifu katika serikali yetu, na maeneo ambayo viongozi wetu wanakutana, na kupitisha sheria na kufanya maamuzi, ili kutuhakikishia kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu? (Yohana.16:8-11)

Baba tunajua ya kwamba kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho (Waefeso.6:12). Kama kanisa tunaiombea serikali yetu ulinzi dhidi ya nguvu katika ulimwengu huu wa giza ili kwamba viongozi wetu wasijihushishe katika uchawi, ibada za sanamu au aina ye yote ya ushirikina. Uturehemu. Tunaomba kwamba waweze kukutii Wewe. Kama kanisa tunampinga Shetani anapotaka kushambulia, kutega na kuirubuni serikali (Yakobo 4:7). Baba, silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome; tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo; tena tukiwa tayari kupatiliza maasi yote, kutii kwetu kutakapotimia (2 Wakorintho.10:4-6).

Tuomba kwa kanisa ambalo litahubiri Injili kinabii kwa serikali; kanisa ambalo litakuwa tayari, wakati ufaao na wakti uisiofaa, kukaripia, kukemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho (2 Timotheo.4:2).

Saa ya 20: Saa 1:00- 2:00 Usiku

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea na usomaji wa Biblia)

Usomaji wa Biblia: Saa la Tano la usomaji wa Zaburi – angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Nguvu ya Neno la Mungu

Hapo mwanzo palikuwapo NENO naye NENO alikuwapo kwa Mungu, naye NENO alikuwa Mungu (Yohana 1:1). Kwa NENO la Bwana mbingu zilifanyika (Zaburi.33:6) na ukivichukua vyote kwa nguvu ya NENO lako (Heb.1:3). Ee Bwana, NENO lako lasimama imara mbinguni hata milele (Zaburi 119:89) kwa maana umelikuza NENO lako kuliko Jina lako lote (Zaburi.138:2). Maana NENO lako li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo (Waebrania.4:12). NENO lako ni kama moto, na kama nyundo ivunjayo mawe vipande vipande (Yeremia 23:29). Neno lako ni upanga wa Roho (Waefeso 6:17) Ndivyo litakavyokuwa NENO lako, litokalo katika kinywa chako; halitakurudia bure bali litatimiza mapenzi yako, nalo litafanikiwa katika mambo yale uliyolituma (Isaya.55:11).

Unajifunua mwenyewe kupitia NENO lako (1 Samweli.3:21), Funua akili zangu nipate kuelewa maandiko (Luka 24:45) Unipatie roho ya hekima na ya ufunuo katika kukujua Wewe (Waefeso.1: 17). NENO lako ni taa ya miguu yangu na mwanga wa njia yangu (Zaburi.119:105) na kufananusha MANENO yako kwatia nuru, na kumfahamisha mjinga. (Zaburi.119:130). Uzielekeze hatua zangu kwa NENO lako uovu usije ukanimiliki (Zaburi.119:133). Una MANENO ya uzima wa milele (Yohana 6:68) na MANENO uliyotuambia ni roho, tena ni uzima (Yohana 6:63). NENO lako lanifariji (Zaburi.119:15) na ninaishi katika kila NENO litokalo katika kinywa chako (Kum ya Torati.8:3; Mathayo.4:4). NENO lako nimelificha moyoni mwangu ili nisikutende dhambi (Zaburi.119: 11). Ninakushukuru kwa kuwa NENO lako linanitakasa (Yohana 15:3; Waefeso.5:26), na njia yangu itasafishika kama nitatii, nikilifuata NENO lako (Zaburi.119:9). Wewe hulituma NENO lako kutuponya, na kututoa katika maangamizo yetu (Zaburi.107:20). Nimelingojea na kulitumainia NENO lako (Zaburi.119: 81,144).

Jumla ya NENO lako ni kweli, na kila hukumu ya haki yako ni ya milele na kwa kupitia NENO lako ninatakasika (Zaburi.119:160; Yohana 17:17). MANENO yako ni MANENO safi ni fedha iliyojaribiwa kalibuni juu ya nchi; iliyosafishwa mara saba (Zaburi.12:6); Nina kuamini Wewe kwa sababu MANENO yako

yamehakikishwa (2 Samweli.22:31). MANENO yako ni matamu sana kwangu, kupita asali kinywani mwangu; nilipoyapata MANENO yako niliyala na yakaleta furaha moyoni mwangu (Zaburi.119:103). Sheria ya Bwana ni kamilifu, Huiburudisha nafsi. Ushuhuda wa Bwana ni amini, humtia mjinga hekima. Maagizo ya Bwana ni ya adili, huufurahisha moyo. Amri ya Bwana ni safi, huyatia macho nuru. Kicho cha Bwana ni kitakatifu kinadumu milele. Hukumu za Bwana ni kweli, zina haki kabisa. Ni za kutamanika kuliko dhahabu, kuliko wingi wa dhahabu safi. Nazo ni tamu kuliko asali, kuliko sega la asali. Tena mtumishi wako huonywa kwazo, katika kuzishika kuna thawabu nyingi. (Zaburi 19:7-11).

NENO la Kristo na likae kwa wingi ndani mwangu ili niweze kuwafundisha na kuwafariji wengine (Wakolosai.3:16) na kumshinda yule mwovu (1Yohana 2:14). Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa natamani maziwa ya akili yasiyogoshiwa, ili kwa hayo tupate kuukulia wokovu (1Petro.2:2). Nakusikia kwa NENO kulete imani katika moyo wangu (Warumi.10:17) ili niweze kukupendeza (Waebrania.11:6). Bwana Yesu Kristo, NENO la Mungu liishilo, Wewe ni Njia, Kweli na Uzima (Yohana 14:6). Na NENO lako likae ndani yangu, nami nikae ndani yako, na nitapokea ninachoomba kwako (Yohana 15:7).

Liimarishe NENO lako katika miji yetu na mataifa, na lizidi na kushinda kwa nguvu (Matendo 19:20). "Maana, mwili wote ni kama majani, na fahari yake yote ni kama ua la majani; bali NENO la Bwana hudumu hata milele." (1Petro1:24,25)

Saa ya 21: Saa 2:00-3:00 Usiku

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea na usomaji wa Biblia)

Usomaji wa Biblia: Saa la Sita la usomaji wa Zaburi – angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Mweleke wa tangazo hili ni: Kupinga uovu

Baba wa Mbinguni, Ni makusudi yako ya milele, uliyoyatimiza katika Yesu Kristo Bwana wetu, kwamba kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho (Waefeso.3: 10). Yeye umempaka mafuta kuwahubiri maskini habari njema, kuwaponya waliovunjika mioyo, kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru walioteswa (Luka 4:18); na wakati alipokuwa hapa duniani alizunguka hiko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi (Matendo 10:38). Baba, Uliigongomea ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, msalabani, ukuusha kuzivua enzi na mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri (Wakolosai.2:13-15). Umempa Mwanao mamlaka yote mbinguni na hapa duniani, kwamba katika Jina la Yesu, kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri Yeye ni Bwana (Mathayo.28:18-20; Wafilipil.2:10,11).

Baba wa utukufu, umemfufua Yesu Kristo kutoka katika wafu na ukamketisha mkono wako wa kuume katika ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jila litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; ukavitia vitu vyote chini ya miguu yake, ukamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote. (Waefeso.1:20-23). Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za ibilisi (1Yohana 3:8). Ahsante kwamba kupitia damu ya Yesu Kristo, ambaye tuna ukombozi, na masamaha ya dhambi, pia ulituokoa katika nguvu za giza, ukatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lako (Wakolosai.1:13-14). Na, kupitia kifo cha Yesu Kristo, Yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani Ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa (Waebrania.2:14-15). Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa Yeye aliyetupenda. Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliopo, wala yatakayokuwepo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kingine cho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana Wetu (Warumi 8:37-39).

Bwana Yesu Kristo, kichwa cha kanisa, umetupa mamlaka dhidi ya nguvu zote za adui kiasi kwamba roho hizo zinatutii (Luka 10:19-20). Umetupa amri kwenda katika katika mataifa na habari njema, kufungua macho ya wasio amini, ili kuwageuza kutoka katika giza kuja kwenye nuru, na kutoka katika nguvu za ibilisi kuja kwa Mungu, ili nao waweze kupokea msamaha wa dhambi na urithi kati ya hao waliotakaswa kwa imani katika Wewe (Luka 9:1-2; Mathayo.28: 18,19; Matendo 26:17,18). Maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome; tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtiii Kristo (2Wakorintho.10: 4,5). Hivyo tunaomba, Mungu wa amani umsete shetani chini ya miguu yetu upesi (Warumi 16:20). Ahsante kwa kutupa silaha zote za Mungu, tupate kuweza kuzipinga hila za shetani, kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Tunasimama siku hii ya uovu, huku tukiwa tumejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani, na kufungiwa miguu utayari tuupatao kwa Injili ya amani; zaidi ya yote tukitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo twaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena tukipokea chepeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu, tunapoomba na kumpinga yule mwovu (Waefeso 6:10-18; Yakobo.4:7; 1Petro.5:9). Tutashinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wetu, ambao hatutapenda maisha yetu hata kufa (Ufunuo 12:11). Yeye aliye ndani yetu ni mkuu kuliko yule aliye duniani (1Yohana 4:4).

Tunaomba sasa, Baba, katika Jina la Yesu Kristo, ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho, tunapokiri kwamba Yesu Kristo ni mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana (Waefeso 3:10; Wafilipi 2:10; Ufunuo.19:16).

Saa ya 22: Saa 3:00 – 4:00 Usiku

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea na usomaji wa Biblia)

Usomaji wa Biblia: Soma toka Mwanzo hadi Ufunuo - angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Lengo la tamko hili ni: Ubaba wa Mungu

Baba wa milele, Wewe ni Muumbaji wetu na umetufanya (Kumbukumbu ya Torati.32:6). Tunatangaza: Wewe ni Baba yetu, Mungu wetu, Mwokozi wetu, Mwamba wetu, Mkombozi wetu na tangu milele ndilo jina lako (Zaburi.89:26; Isaya.63:16). Sisi tu udongo, nawe u mfinyanzi wetu; sisi sote tu kazi ya mikono yako (Isaya.64:8). Hivyo, tnaungana na mamilioni ya watu dunia pote na tunakiri: Tunaamini katika Mungu Baba, Mwenyezi, muumba wa mbingu na nchi. Tunakushukuru kwa ahadi yako ya agano kwamba utakuwa Baba kwetu; nasi tutakuwa kwako wanao wa kiume na wa kike (2 Wakorintho 6:18). Baba yetu wa Mbinguni, Jina lako litukuzwe, ufalme wako uje na mapenzi yako yatendeke hapa duniani kama yanavyotendeka huko mbinguni (Mathayo.6:9-10). Mwanao Yesu Kristo alikufunua Wewe ulimwenguni (Mathayo.11:27). Jidhihirishe kwa kanisa na ulimwenguni kama Mungu wa mianga, ambaye kila karama njema iliyo kamili inatoka, kwako hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka. (Yakobo 1:17).

Wote na tuwe wamoja; kama wewe, Baba, na Mwana mlivyo wamoja (Yohana14:20; 17:21). Tunataka kujujua Wewe kama ulivyo na tunataka kulitukuza jina lako kama Mwana wako Yesu alivyolikutukuza, na tunataka kukujua Wewe uliye tangu mwanzo, Wewe uliyepo, na uliyekuwapo na Yeye ajaye (1 Yohana 2:13-14; Yohana 17:1-3). Kama Ibrahimu na Musa uliyezungumza nawe uso kwa uso, tunataka kuishi katika mahusiano ya uso kwa uso na Wewe.

Baba, tunapokea kurudiwa kwetu katika maisha yetu kwa sababu unatupenda na kutuhesabu watoto wa kiume na wa kike. Tunanyenyekeza roho zetu kwako kwa ajili ya kurudiwa kwa faida yetu wenyewe ili tuweze kushiriki utakatifu wako. Tunajua ya kwamba kurudiwa kwetu kutaleta mavuno ya haki na amani kwa wale waliozoezwa kwayo (Waebrania.12:6-11). Kama mwana amheshimuvyo baba yake na mtumishi humcha bwana wake tunataka kukucha na kukuheshimu (Malaki.1:6). Na kama Mwana Yesu alivyokutukuza Wewe ulimwenguni, pia ni haja ya moyo wetu kukutukuza Wewe ulimwenguni (Yohana 17:4).

Baba wa yatima na mwamuzi wa wajane, Mungu katika kao Lake takatifu (Zaburi.68:5). Kama vile baba awahurumiavyo watoto wake, pia Wewe umewahurumia wale wakuchao (Zaburi.103:13). Kwa kuwa tu wana, Mungu ulimtuma Roho wa Mwana wake mioyoni mwetu, ambayo kwa hiyo twalia “Aba, yaani Baba!” Kwa kuwa hatukupokea tena roho ya utumwa iletayo hofu; bali tulipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani Baba, tukijua ya kuwa tu warithi; warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo; naam, tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye. (Wagalatia.4:5-7; Warumi.8:15,17). Kwa sababu tunaamini kwamba tu wana wa Ibrahimu na kama ulivyo ahidi kwa Ibrahimu kwamba mataifa yote yatabarikiwa kupitia yeye, tunaomba pia kwamba utufanye kuwa baraka kwa mataifa. Neno lako kwa uwazi kabisa lasema, Basi hao walio wa imani hubarikiwa pamoja na Ibrahimu, aliyekuwa mwenye imani (Wagalatia.3:6-10).

Tunataka kuwa waabudu wa kweli, hivyo tufundishe, Baba, tukuabudu katika roho na kweli (Yohana 4:23). Ulitufundisha kwamba Mwana hawezi kufanya lolote mwenyewe; atafanya lile tu alionalo Baba akifanya, kwa sababu lolote Baba afanyalo, ndilo hilo Mwana hufanya (Yohana 5:19) Hivyo Baba, tufunulie lile ambalo unataka tufanye ili tulifanye.

Maombi haya yaombwe na Wababa tu

Tunapiga magoti mbele zako, Baba. Kwa jina lako ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unataitwa (Waefeso.3:14-15). Baba, tusaidie kama wababa wa duniani tusiwachokoze watoto wetu, kwamba wasije kukata tamaa. Utusaidie kuwarudi na kuwalea katika adabu na maonyo ya Bwana (Waefeso.6:4: Wakolosai.3:21). Badilisha mioyo yetu wababa kwa watoto wetu na mioyo ya watoto wetu kwa sisi wababa wao katika siku zetu na kuwatilia waasi akili za wenye haki, na kumwelekea Bwana tayari watu waliotengenezwa, ili usije ukaipiga dunia kwa laana (Luka 1:17; Malaki.4:6). Kama wababa, tunawabariki watoto wetu kama Isaka na Yakobo walivyowabariki watoto wao (Mwanzo.27& 49). Katika Jina lako tunafanya matamko hayo mbele ya watoto wetu: “Bwana awabariki na kuwalinda, Bwana awaangazie nuru za uso wake, na kuwahifadhi; Bwana awainulie uso wake na kuwapa amani!” (Hesabu 6:24-26). Baba utusaidie kuwa na rehema kama vile Wewe ulivyo na rehema (Luka 6:23-26). Tunawaombea watoto wetu kwamba wawaheshimu Baba zao na Mama zao, ili siku zao zipate kuwa nyingi, katika nchi uliowapatia (Kutoka.20:12). Baba, makusudi yako katika ndoa ni kuleta kizazi kinachokucha Wewe. Tunakusihi utusaidie kutimiza makusudi hayo Yako (Malaki.2:15). Kama wa baba tunakiri kwamba katika matukio mengi hatujawa waaminifu katika maagano ya ndoa zetu. Tunakiri kwamba mara nyingi mafanikio, kutimiza matakwa yetu na kufukuzia fedha na heshima kumesababisha kuwaacha watoto wetu. Tunakiri

kwamba mara nyingi tumesababisha maumivu na fedheha kwa wake zetu na watoto wetu. Tunakiri kwamba kama wababa tumeshindwa kiasi cha watoto wetu kushindwa kufikia ujuzi wa ukamilifu na uelewa wa Ubaba wako. Tunaomba utusamehe katika Jina la Yesu. Amina.

Saa ya 23: Saa 4:00 – 5:00 Usiku

(Omba maombi yako binafsi na tamka (proclaim) lengo la saa hii kabla ya kuendelea na usomaji wa Biblia)

Usomaji wa Biblia: Soma toka Mwanzo hadi Ufunuo - angalia daftari la kumbukumbu kujua mahali pa kuanzia kusoma

Mwelekeo wa tanganzo hili ni: Kuwaombea wasio amini/waliopotea

Baba, Ufalme wako na uje, na mapenzi yako yatendeke hapa duniani kama yanavyotendeka huko Mbinguni (Mathayo.6:10). Kama warithi pamoja na Kristo Yesu, tunaomba mataifa kuwa urithi wetu na miisho ya dunia kuwa milki yetu (Mwanzo.2:8; Warumi.8:17). Tunaomba kwa wokovu wa watu kutoka katika kila taifa, kabila, watu na lugha- kwamba uwingi wa watu siku moja wasimame mbele za kiti chako mbele za Mwana-Kondoo (Ufunuo.7:9).

Uliupenda ulimwengu sana hata ukamtoa Mwanao pekee, ili kila amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele. Hukumtuma Mwanao ulimwenguni kuuhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe kupitia Mwanao (Yohana.3: 16-17). Tumepatanishwa na Wewe kupitia Kristo na Umetupa huduma ya upatanisho (2 Wakorintho.5:18-19). Tunaombea mataifa ya dunia na marafiki zetu wapendwa wapatanishwe nawe. Hupendezwi na kifo cha mwenye dhambi, unapendezwa wanapo zugeuka njia zao (Ezekieli.18:23).

Bwana Yesu, Wewe ni Mwana-Kondoo wa Mungu, uzichukuaye dhambi za ulimwengu! (1 Yohana 1:9). Igeuze mioyo ya mataifa kwako ili wakugeukie (Maombolezo 5:21). Kupitia nguvu za Roho Mtakatifu tunaomba uhakikishe dhamira ya ulimwengu kwa habari ya dhambi na haki na hukumu (Yohana16:8).

Tunataka kuwatumikia watu angali muda upo wakufanya kazi (Yeremia.8:20; Mithali.10:5). Maelfu katika kanisa lako na waitikie unapoita: “Nani nitakaye mtuma? Wawe tayari kwenda. Na waseme kama alivyosema Isaya: “Nipo hapa nitume mimi!” (Isaya.6:8). Tunaomba kwamba mavuno ni mengi bali watenda kazi ni wachache. Hivyo tunakuomba Wewe Bwana wa mavuno, utume watenda kazi katika mavuno yako (Mathayo.9:37-38). Wakristo ulimwengu kote wainue macho yao kuyatazama mashamba, ya kuwa yamekwisha kuwa meupe, tayari kwa mavuno (Yohana 4:35). Na kanisa lako lipate kusikia kwa namna mpya kwamba wito wetu ni kwenda ulimwenguni kote na kuhubiri Injili kwa kila kiumbe (Marko 16:15). Mamlaka yote umepewa Wewe, Bwana Yesu Kristo. Umetuamuru tufanye mataifa yote kuwa wanafunzi na kuwafundisha kuyashika yote uliyotuamuru sisi; na tazama, wewe upo pamoja nasi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari (Mathayo.28:18-20).

Bwana, utuwezeshe watumishi wako duniani kote kulinena neno lako kwa ujasiri wote (Matendo 4:29). Utujalie sisi ahadi yako kwamba “tutapokea nguvu Roho Mtakatifu atakapo tujilia, na tutakuwa mashahidi wako; Yerusalemu, na Judea yote na Samaria, na hata mwisho wa dunia.” (Matendo 1:8). Umetuweka leo juu ya mataifa na juu ya falme, ili kung’oa na kubomoa, na kuharibu, na kuangamiza; ili kujenga na kupanda. Tunataka kuona ufalme wako ukiendelea ulimwenguni kote (Yeremia.1:10). Bwana Mungu, tunakuomba kwamba utende ishara na ajabu na nguvu za namna nyingi, na kwa magawanyo ya Roho Mtakatifu, kama upendavyo Mwenyewe (Waebrania.2:4). Tunaomba kwamba Injili ya wokovu na upatanisho na Mungu inenwe kwa kazi na kuheshimiwa. Tuokoe kutoka kwa watu waovu wanaopinga kazi yako (2 Wathesalonike.3:1-2). Baba, tufungulie mlango kwa lile neno lako, tuinene siri ya Kristo, kwa uwazi kwa watu wote (Wakolosai.4:3-4). Tunaomba kwamba tupewe usemi kwa kufumbua vinywa vyetu, ili tuhubiri kwa ujasiri ile siri ya Injili (Waefeso.6:19-20). Tunaomba kwa mavuno makubwa – na mbegu tuipandayo ianguke katika udongo mzuri na kuzaa matunda, mia, na sitini, na thelathini.” (Mathayo.13:23)

Bwana Yesu, hukuja ulimwenguni ili utumikiwe, bali kutumika na kutoa uhai wako kama dhabihu kwa mataifa na wasiookoka (Marko.10:45). Bwana hukawii kuitimiza ahadi yako, kama wengne wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia maana hupendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba (2 Petro.3:9). Ulijeruhiwa kwa makosa yetu, ulichubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yako, na kwa kupigwa kwako sisi tumepona (Isaya.53: 5). Hivyo tuna ujasiri kukukaribia kwa kuwa tunajua ya kwamba tukiomba lo lote sawasawa na mapenzi Yako, utasikia na tunajua ya kwamba tutapata tuombayo. Na Bwana tunakuomba Wewe wokovu wa mataifa (1 Yohana.5:14-15). Mungu Mwenyezi, umemwadhimisha mwanao mno na ukamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA kwa utukufu wa Mungu Baba (Wafilipi.2:9-11).

Saa ya 24: Saa 5:00 – 6:00 Usiku

(Omba maombi yako binafsi na tamla lengo la tamko hili kabla ya kuendelea na usomaji wa Biblia)

Usomaji wa Biblia: Soma toka Mwanzo hadi Ufunuo - consult log-book kwa maali pa kuanzia

Lengo la tamko hili ni: Ufalme wa Mungu

Baba, tunaomba kwamba Ufalme wako uje na mapenzi yako yafanyike hapa dunia kama yanavyofanyika Mbinguni (Mathayo.6:9,10). Wewe ni Mfalme wa dunia hii, na kama kanisa katika mataifa tunakuja kukuabudu. Wewe unatawala juu ya mataifa (Zaburi.22:27,28). Kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele, Fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya adili (Zaburi.45:6). Kutoka mataifa yote tutaunena utukufu wa ufalme wako, na kuuhadithia uweza wako. Ili kuwajulisha watu matendo yako makuu, na utukufu wa fahari ya ufalme wako. Ufalme wako ni ufalme wa zamani zote, na mamlaka yako ni ya vizazi vyote (Zaburi 145:11-13).

Maana kwa ajili yetu Mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanaume; na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani. Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe, katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; kuuthibitisha na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele (Isaya.9:6,7). Utusamehe kwa kuangalia sana mahitaji yetu na kujenga falme zetu wenyewe, na kuacha kujenga sehemu ya la Wewe kukaa katika mataifa (Hagai.1:4-8). Tafadhali fungua macho ya mioyo yetu yatiwe nuru, tujue tumaini la mweito wake jinsi lililvyo; na utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake; aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia (Waefeso.1:18-21). Tunapiga magoti na kutambua mamlaka yaliyo katika Jina la Yesu na kukiri kwamba Yesu Kristo ni Bwana (Wafilipi.2: 10-11).

Tunaomba kwamba waumini wengi zaidi wasikie neno la Injili ya ufalme, na mbegu itaanguka katika mioyo iliyoandaliwa, ili kwamba kuwa na mavuno makubwa ya roho katika kizazi chetu (Mathayo.13:3-23).

Tunakubariki, Mungu mkuu, na tunakusifu na kukuheshimu Wewe uishiye milele; kwa maana mamlaka yako ni mamlaka ya milele, na ufalme wako hudumu toka

kizazi hata kizazi (Danieli.4:34). Tunatangaza kwamba utakuja muda ambao viti vya enzi vitawekwa; na mmoja aliye mzee wa siku ameketi; mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama sufu safi; kit chake cha enzi kilikuwa miali ya moto, na gurudumu zake moto uwakao. Mto kama wa moto ukatoka ukapita mbele zake; maelfu elfu wakamtumikia, na elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele zake; hukumu ikawekwa, na vitabu vikafunuliwa. Na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu akamkaribia huyo mzee wa usiku, wakamleta karibu naye. Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, ambayo haitapita kamwe, na ufalme wake ni ufalme usioweza kuangamizwa. Na watakatifu wako uliye juu wataupokea ufalme, na kuumiliki huo ufalme milele, naam hata milele na milele (Danieli.7:9,10,13,14,18). Tunaungana na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi ya juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, tukisema: “Baraka na heshima na utukufu na uweza una yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele!” (Ufunuo.5:13)

Tunatangaza sasa kwa mataifa yote: “Inueni vichwa vyenu, enyi malango, Inukeni, enyi malango ya milele, Mfalme wa utukufu apate kuingia!” (Zaburi 24:7)